**DEREVA** bajaji mbaroni madai kuua mgambo kwa kisu kikatili

UKURASA 7



**MPANGO** ataja mbinu kukuza rasilimali watu imara Afrika

UKURASA 2




Wananchi wanapohisi Tume Haki Jinai ina kazi kubwa kuwarekebisha polisi

Na Mwandishi Wetu

KUTOKA Dodoma, Dar es Salaam, Tanga hadi Tabora, kila Mtanzania akiulizwa ana la kusema kuhusu polisi ambao wanaweza kuwa wahusika wakuu kwenye mabadiliko ya taasisi za utoaji haki jinai.

Rais Samia Suluhu Hassan, ameunda Tume ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai, ambayo hivi karibuni imekabidhi ripoti yake na sasa inajipanga kuyafanyia kazi mapendekezo yake kuhusu namna bora ya kuwahudumia na kuwatendea haki wahalifu wa makosa ya jinai.

UKURASA 11

# Nipashe

Jumatano Julai 26, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581383

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian...

# Bei bidhaa za ujenzi zashtua



Dk. Ashatu Kijaji

**WAZIRI** akiri hali mbaya, atoa maagizo....

*Endelea Ukurasa wa 3*

**RIPOTI YA HAKI JINAI**

## LHRC yaibuka na hoja tano nyeti kwa serikali

UKURASA 7

## Rais Samia: Tusikubali kugawanyika kwa kisingizio chochote kile

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akiweka silaha za jadi; mkuki na ngao kwenye mnara wa mashujaa katika maadhimisho ya Siku ya Kumbukumbu ya Mashujaa, Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

**MICHEZO** **GAMONDI AVIMBA DROO MICHUANO CAF** UK. 24 **KATUNI** UK. 6

# ‘Tusikubali kugawanyika kwa kisingizio chochote’

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ameweka jiwe la msingi katika ujenzi wa Mnara na Uwanja mpya wa Kumbukumbu ya Mashujaa kwenye Mji wa Serikali Mtumba, akiwataka Watanzania kuwa wamoja na kutokubali mtu au kikundi chochote kuwagawa kwa kisingizio chochote kile.

Aliagiza hayo jana jijini hapa alipohutubia katika maadhimisho ya Siku ya Mashujaa iliyofanyika kwa mara ya kwanza katika viwanja hivyo vilivyoko Mji wa Serikali Mtumba jijini.

“Ndugu zangu nitoe wito kwa Watanzania wote kuenzi mashujaa wetu kwa kudumisha amani, umoja, mshikamano na utulivu wa nchi yetu na kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya maendeleo ya taifa letu.

“Kamwe tusikubali mtu yeyote au kikundi fulani cha watu kitugawe kwa kisingizio chochote kile. Tanzania ni moja na kamwe haitogawanyika,” alisisitiza Rais Samia.

Mkuu wa Nchi pia aliagiza Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na wahusika wengine wote kuendelea kusimamia kwa karibu ujenzi wa mnara na uwanja huo pamoja na miundombinu mingine yote ili ikamilike kwa wakati na kwa viwango vilivyokusudiwa.

“Vilevile, Wizara ya Fedha ihakikishe inatoa fedha kwa kuzingatia mpangokazi wa ujenzi huu na kusiwe na ucheleweshaji wowote,” Rais Samia aliagiza.

Alisema lengo la maadhimisho hayo ni kutoa heshima kwa mashujaa walioipigania nchi na kujikumbusha historia ya taifa.

“Kukamilika kwa uwanja huu kutaendelea kuongeza heshima ya makao makuu ya nchi na nipongeze Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma kwa kusimamia vizuri awamu ya hii ya kwanza ya ujenzi wa Uwanja wa Mashujaa.

“Nilipofika hapa nilionyeshwa ramani ya uwanja, nimevutiwa sana. Uwanja huu ukimalika utakuwa na sehemu ya migahawa ya kimataifa, kumbi za mikutano na vivutio vya watu kupumzika na kupata burudani mbalimbali na mnara wetu ukimalika utakuwa ni mnara mrefu namba moja barani Afrika,” alisema.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, alisema ujenzi wa mnara na uwanja huo ni sehemu ya utekelezaji wa agizo la Rais kuwa na eneo linaloendana na hadhi ya makao makuu ya nchi.

“Mheshimiwa Rais muda mfupi umeweka jiwe la msingi la ujenzi wa mnara pamoja na Uwanja wa Mashujaa katika mji huu wa kiserikali Mtumba, lakini hii yote ni matokeo ya agizo lako ulilolitoa Julai 25, mwaka jana katika Uwanja wa Mashujaa ulioko eneo la Jamatini,” alisema.

Waziri huyo alisema Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia mkandarasi SumaJKT na mshauri elekezi, Chuo Kikuu cha Ardhi wanaendelea kukamilisha ujenzi wa mnara na uwanja huo kwa awamu ya kwanza.

“Mradi huu utakuwa na miradi mingine miwili unganishi ukiwamo ujenzi wa mnara wa Mji wa Serikali Mtumba wenye urefu wa mita zaidi ya 110 ambao ukikamilika utakuwa mrefu zaidi barani Afrika. Utakuwa kivutio cha utalii na kutoa fursa za kiuchumi kwa wakazi wa Dodoma na Tanzania kwa ujumla,” alisema.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa barabara ya Inyala-Simambwe yenye urefu wa kilomita 16.7 katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya juzi. Barabara hiyo ni miongoni mwa miradi inayofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU). **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mpango ataja mbinu kukuza rasilimali watu imara Afrika

**Na Romana Mallya**

MAKAMU wa Rais, Dk. Phillip Mpango, amesema taasisi za fedha za kikanda na kimataifa, zinapaswa kufadhili ajenda ya Afrika ya rasilimali watu imara ili kutatua changamoto zinazolikumba bara hilo.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua kikao cha mawaziri wa kisekta katika mkutano wa wakuu wa nchi kuhusu rasilimali watu, Dk. Mpango pia alitoa wito kwa wataalamu kujadili namna bora ambayo sekta binafsi inaweza kuhamasishwa kikamilifu.

Pia alitoa wito kwa washiriki kujadili na kuweka mkazo kwenye sekta ya afya kwa kuangalia masuala ya lishe na kuwataka wataalamu kujikita katika sekta muhimu ambazo hazijatiliwa mkazo ili ziboreshwe na kuwa na tija katika uwekezaji wa rasilimali watu wenye afya na lishe bora, ujuzi, teknolojia na maarifa katika kuleta ushindani duniani.

“Uwekezaji wa rasilimali watu ni wa muda mrefu, hivyo unahitaji ufadhili wa gharama nafuu na ukomavu wa muda mrefu. Sekta binafsi ni mnufaika mkuu wa juhudi za maendeleo ya rasilimali watu, kwa hiyo ushiriki wake ni muhimu,” alisema.

Dk. Mpango alisema taasisi za mafunzo, zikiwa wahusika wakuu katika maendeleo ya mtaji wa watu, zinaweza na zinapaswa kusaidia kuimarisha uwezo wa ndani ili kusimamia na kutumia rasilimali kwa ufanisi.

Kdhalika, alisema nchi za Afrika zinapaswa kutumia mkutano huo kujadili na kutoka na azimio la kuboresha malengo katika kuwekeza kwenye rasilimali watu hasa vijana ambao hao ndio injini ya ukuaji uchumi na maendeleo.

Alisema mkutano huo ni fursa kwa mataifa ya Afrika katika kujadiliana namna ya kuwekeza katika mtaji wa rasilimali watu wa vijana kwa kuwa ndilo bara linalotabiriwa kuwa na mtaji mkubwa zaidi wa nguvu kazi duniani miaka michache ijayo.

“Ili kufikia huko kwa kuwa na mtaji wa rasilimali watu vijana, ni lazima changamoto kubwa zilizoko sekta mbalimbali ziboreshwe zikiwamo elimu, afya, miundombinu, teknolojia na ujuzi,”' alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Mpango, ajenda ya Afrika ni kuwa zaidi ya asilimia 70 ya watoto wapate elimu kuanzia ya awali hadi chuo kikuu na malengo iliyojiwekea ni ifikapo 2025, iwe imefikiwa na mataifa hayo.

Alikumbusha kuwa wana muda mfupi kufikia azma hiyo na kwamba kupitia mkutano huo muhimu wa kujadili agenda ya mtaji wa rasilimali watu, wajadiliane namna ya kuboresha na kufikia lengo lao.

Dk. Mpango alisema takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 40 ya watu wenye umri kati ya miaka 0 hadi 14 kutoka nchi za kipato cha chini waliopata elimu watatoka nchi za Afrika ifikapo mwaka 2050 na kutaka uwekezaji kwa vijana ili wawe na ujuzi na maarifa.

Nchi zilizopiga hatua kimaendeleo na uchumi, alisema ziliwekeza kwenye mtaji wa rasilimali watu, hivyo hakuna budi kuona umuhimu wa kufanya hivyo.

Aliueleza mkutano huo kuwa Tanzania imechukua hatua katika kuboresha sekta mbalimbali kwa kuongeza bajeti katika elimu, afya, kilimo, miundombinu na huduma za jamii ili kuboresha huduma na kuwa na taifa lenye watu wenye afya bora, elimu na ujuzi.

Pia alisema Tanzania inaendelea kuboresha huduma za afya na imenunua vifaa tiba na kutolea mfano mashine za MRI na kuziboresha huduma za kibingwa na kupunguza vifo vya watoto wachanga kutoka 67 kwa kila vizazi hai 1,000 hadi kufikia vifo 47 kwa kizazi hai 1,000 mwaka jana.

Katika sekta ya elimu kiongozi huyo alisema serikali imefanikiwa kutoa elimu bila ada kuanzia ngazi ya msingi hadi sekondari na kuongeza usajili wa wanafunzi wanaoanza elimu ya msingi kutoka asilimia 85 miaka kadhaa iliyopita hadi kufikia asilimia 97 ya sasa.

Kadhalika alisema kiwango cha wanafunzi wanaomaliza elimu ya msingi na kuendelea na elimu ya sekondari imeongezeka kwa zaidi ya asilimia 90.

Pia alisema serikali iko kwenye mapitio ya Sera ya Elimu ili kuiboresha na kuja na sera mpya itakayowaandaa wanafunzi kupata ujuzi zaidi wa kujiajiri badala ya kusoma kwa lengo la kusubiri kuajiriwa.

Aidha alisema Tanzania imepiga hatua kwenye teknolojia na matumizi ya kidigiti ambayo yameongezeka kutoka asilimia 30 miaka kadhaa iliyopita hadi 48 ya sasa.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema Tanzania imepiga hatua kubwa katika kuongeza kasi ya matokeo ya rasilimali watu na kuwawezesha vijana kuwa na maarifa na ujuzi unaohitajika.

“Tumeoanisha programu za elimu na mafunzo ya ufundi stadi na mahitaji ya viwanda, kutengeneza njia jumuishi kutoka elimu hadi ajira na tunabuni programu ambazo zitawaandaa wahitimu wa ngazi zote, hata walioacha shule ili kuchangamkia fursa na kuchangia ipasavyo kwa nguvu kazi,” alisema.

Naibu Waziri Mkuu wa Cape Verde, Dk. Olovo Correla, alisema ili kutatua changamoto za rasilimali watu, nchi za Afrika zinapaswa kujadili namna ya kupunguza umaskini kwenye nchi zao.

Alisema vijana wengi wanakimbia nchi za Afrika kutokana na kukosekana kwa fursa kwenye nchi zao.

“Bara lina watu wengi hasa vijana lakini kumekuwa na changamoto nyingi zikiwamo elimu, afya, ajira na miundombinu. Ili kuendeleza katika rasilimali watu lazima tubadilike,” alisema.

Dk. Correla alisema Waafrika wanapaswa kuishi kwa utu kwa kuwa ndani ya Afrika kuna kitu, hivyo washikamane kuondoa umaskini na kuboresha rasilimali watu.

HABARI KITAIFA

## Kinana: Waliohodhi ardhi ya uwekezaji wanyang'anywe

**Na Beatrice Shayo,** BABATI

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Kanali mstaafu Abdulrahman Kinana, amesema kuna baadhi ya wawekezaji wamepewa ardhi kuzalisha lakini wanakodisha.

Amesema kitendo hicho ni 'unyonyaji' na atakwenda kukutana na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula kutatua changamoto hiyo.

Katika mkutano wa hadhara Kata ya Dareda wilayani Babati, mkoani Manyara jana, Kinana alisema amepokea taarifa ya maendeleo ikiwa na mambo manne kutoka kwa Mbunge wa Babati Vijijini (CCM), Daniel Sillo, hivyo atawasiliana na mawaziri husika kupata ufumbuzi.

Kinana alisema kama kuna maeneo ambayo 'yamekaa bure' na watu waliopewa hawayatumii, hawana haki ya kuendelea kuyashikilia.

"Mbunge wenu tatizo la kwanza alilonipa - kuna maeneo ambayo wamepewa watu wanaitwa wawekezaji. Mimi ninajua mwekezaji wa kwanza ni mtu anayewekeza nguvu na jasho lake ambaye ni mkulima.

"Kama kuna maeneo yamekaa bure na watu waliopewa hawayatumii, hawana haki ya kukaa nayo. Wiki ijayo, Waziri wa Ardhi atakuja na mimi nitampigia simu nizingumze naye, nitamwambia kuna watu wamekalia maeneo wanajiita wawekezaji hawayatumii na inawezekana wanawakodishia ardhi wananchi," alisema.

Kinana pia alisema amejulishwa kuwapo tatizo linaloendelea kati ya hifadhi na wananchi, hivyo atakwenda kuzungumza na Waziri wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, ili ashughulikie tatizo hilo.

Alisema Mbunge Sillo pia alimweleza kuna barabara inayotoka Dareda kwenda Dongobeshi yenye urefu wa kilometa 60, mpaka sasa imejengwa kilometa nane tu.

Alizitaja changamoto zingine za eneo hilo ni upungufu walimu na watumishi wa kada ya afya. Amemwahidi yote yatashughulikiwa na serikali ya CCM.

Awali akizungumza na wananchi hao, Kinana alisema kuna tatizo kubwa katika kupata huduma ya maji.

Alitumia nafasi hiyo kumhakikishia mfadhili wa mradi wa maji kupitia Mkuu wa Manyara, Queen Sendega, atamlinda na kumwomba aendelee kufanya kazi zake vizuri, aongeze miradi, atanue miradi ya maji, elimu, afya na hakuna atakayemfanyia usumbufu au vurugu zozote.

"Na hapo ndipo unapoona kazi ya CCM, kulikuwa na tatizo mradi wa maji umekwama, wananchi wanalalamika kilichofanyika. Alikuja Katibu Mkuu wa chama mkamweleza. Chama hiki kinatoa maagizo kwa serikali sio serikali kutoa maagizo kwa chama," alitamba.

Alisema chama hicho kinatoa ahadi na kutekeleza huku akikumbusha kuwa zamani hakukuwa na barabara za lami, maji na hata shule zilikuwa chache, lakini sasa mikoa yote imeunganisha na barabara za lami.

Kinana alisema chama hicho kazi yake ni kutenda, akivizodoa vyama vingine kazi kwa madai kwamba wameviachia viendelee kuongea na wao wanaendelea kutenda.



Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, akiweka mkuki na ngao katika mnara wa kumbukumbu wa mashujaa katika maadhimisho ya Siku ya Mashujaa Duniani jijini Arusha jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Serikali yakiri bei juu vifaa ujenzi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema mwenendo wa bei za mazao na chakula zimeshuka huku vifaa vya ujenzi vikipanda kwa Julai ikilinganishwa na mwezi uliopita.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, akitoa taarifa ya mwenendo wa bei za bidhaa muhimu nchini jana, alisema bei ya saruji aina ya 32.5 kwa mwezi Julai ni kati ya Sh. 14,125 na Sh. 23,250 kwa mfuko wa kilo 50.

"Bei ya juu ya saruji hiyo imeongezeka kwa asilimia 0.5 sawa na ongezeko la Sh. 125 kwa mfuko wa kilo 50 ikilinganishwa na bei ya Juni, 2023 ambayo ilikuwa Sh. 23,125 kwa mfuko wa kilo 50," alisema.

Alisema uchambuzi wa wastani wa bei ya saruji aina ya 32.5 nchini unaonyesha kuwa bei yake imepanda kwa asilimia 3.2 ikilinganishwa na wastani wa bei ya bidhaa hiyo kwa mwezi Juni.

"Saruji aina ya 42.5 uchambuzi unaonesha kuwa bei kwa Julai, 2023 ni kati ya Sh. 15,000 na 24,875 kwa mfuko wa kilo 50. Bei ya juu ya saruji hiyo imeongezeka kwa asilimia 1.5 sawa na ongezeko la Sh.375 kwa mfuko wa kilo 50 ikilinganishwa na bei ya mwezi Juni ambayo ilikuwa Sh.24,500 kwa mfuko wa kilo 50," alisema.

Kuhusu mabati, alisema bei ya bati jeupe geji 30 kwa mwezi Julai ni kati ya Sh. 21,500 na 27,000. Alisema bei hiyo imeonesha uhimilivu kwa kutokuwa na mabadiliko yoyote ya juu au ya chini, kulinganisha za bei ya Julai na Juni, 2023.

"Bei ya chini iko katika mkoa wa Iringa wakati bei ya juu ipo katika mkoa wa Manyara,"alisema.

Kuhusu bei ya nondo, alisema milimita 10 kwa mwezi Julai ni kati ya Sh. 11,750 na 18,000 na imeonyesha uhimilivu kwa kutokuwa na mabadiliko yoyote ya bei ya juu au bei ya chini kulinganisha za bei ya Julai na Juni, mwaka huu.

"Bei za chini ziko katika mkoa wa Tabora na bei ya juu ipo katika mkoa wa Iringa. Bei ya nondo mm 12 kwa mwezi Julai 2023 ni kati ya Sh. 22,000 na 28,000. Bei hiyo imeonyesha uhimilivu kwa kutokuwa na mabadiliko yoyote ya bei ya juu au bei ya chini ukilinganisha bei za Julai 2023 na Juni 2023. Bei za chini ziko katika mkoa wa Dar es Salaam na bei ya juu ipo katika mikoa ya Rukwa na Katavi,"alisema.

Pia alisema bei ya sukari kwa mwezi Julai 2023 ni kati ya Sh.2,700 na 3,300 kwa kilo na takwimu zinaonyesha kuwa mwezi Juni sukari iliuzwa kati ya Sh. 2,650 na Sh. 3,133 kwa kilo.

"Kwa mwezi Julai, bei ya chini iko katika mikoa ya Tanga, Singida na Songwe na bei ya juu iko katika mkoa wa Ruvuma.

Ni matumaini yangu kuwa bei hizi zitaendelea kushuka zaidi kwani viwanda vimeshaanza uzalishaji toka mwanzoni mwa Julai, 2023," alisema.

Alieleza kuwa hali ya kuchelewa uzalishaji imesababishwa na kuendelea kunyesha kwa mvua za masika hadi mwishoni mwa Juni, 2023 kwenye maeneo mengi yanayolima miwa.

Dk. Kijaji alisema bei ya mafuta ya kupikia ya alizeti kwa mwezi Julai ni kati ya Sh. 4,000 na 7,500 kwa lita na ni himilivu.

"Bei ya chini ya mafuta ya kupikia ya alizeti inapatikana katika mikoa ya Singida na Kilimanjaro, wakati bei ya juu inapatikana katika mkoa wa Mtwara. Hata hivyo, uchambuzi unaonyesha wastani wa bei ya mafuta ya kupikia ya alizeti kwa mwezi Julai 2023 imeshuka kwa asilimia 5.8 kulinganisha na wastani wa bei ya mafuta hayo kwa mwezi Juni," alisema.

Alisema bei ya unga wa ngano kwa Julai 2023 ni kati ya Sh. 1,900 na 2,300 kwa kilo na imepungua kwa asilimia 4.2 kulinganisha na bei ya juu ya Juni iliyokuwa Sh. 3,400 kwa kilo.

Alifafanua kwa bei ya mahindi kwa Julai ni kati ya Sh. 665 na 1,500 kwa kilo na imeshuka kwa asilimia 3.2 huku bei ikiwa chini kwa mkoa wa Ruvuma na bei ya juu imeonekana katika mikoa ya Pwani, Mtwara na Kilimanjaro.

Kutokana na mwenendo huo wa bei, aliwataka wazalishaji wa bidhaa zote za viwandani kuongeza jitihada za uzalishaji wa bidhaa zenye ubora unaohitajika sokoni na kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa ili kukabiliana na kupanda kwa bei za bidhaa mbalimbali nchini.

"Hatutavumilia kuona mzalishaji, msambazaji au muuzaji wa bidhaa yoyote ile akiongeza bei ya bidhaa yoyote holela bila sababu ya msingi," alisema.

Aliagiza maofisa biashara kwenye halmashauri nchini kuhakikisha wanasimamia ipasavyo eneo hilo la bei za bidhaa ili kuwalinda wazalishaji na walaji.

TANGAZO

Access Microfinance Bank Tanzania

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZISIZOKAGULIWA KWA UMMA

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2023

| | | (Kiasi kwa shilingi milioni) | |
|---|---|---|---|
| | | Robo Mwaka ya sasa 30 JUNI 2023 | Robo Mwaka iliopita 31 MACHI 2023 |
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 4,775 | 5,617 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 8,070 | 5,885 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 226 | 808 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 22 | 69 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 200 | 200 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 52,875 | 50,434 |
| 12 | Mali Nyingine | 8,499 | 8,643 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 788 | 773 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **75,455** | **72,429** |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 700 | 500 |
| 18 | Amana za Wateja | 57,130 | 54,614 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,020 | 821 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 2,108 | 2,028 |
| 27 | Dhima Nyingine | 6,057 | 6,604 |
| 28 | Madeni | - | - |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **67,014** | **64,567** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29)* | **8,441** | **7,863** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 40,000 | 40,000 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (32,537) | (32,537) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 978 | 401 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | 0 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **8,441** | **7,863** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 495 | 369 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 4,782 | 5,444 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 4,783 | 5,260 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 64 | 64 |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 11.19% | 10.86% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 8.29% | 9.77% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 99.70% | 101.05% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 70.07% | 69.63% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 70.34% | 69.91% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 4.93% | 3.16% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 4.18% | 3.26% |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI 2023

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | (Kiasi kwa shilingi milioni) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Jumla |
| **Kipindi cha sasa hadi 30 JUNI 2023** | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka 2023 | 40,000 | - | (32,537) | - | - | 7,463 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 978 | - | - | 978 |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa 30 JUNI 2023** | **40,000** | **-** | **(31,559)** | **-** | **-** | **8,441** |
| **Kipindi cha Mwaka uliopita hadi 31 Disemba 2022** | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka 2022 | 40,000 | - | (33,813) | 229 | - | 6,416 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,047 | - | - | 1,047 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 229 | (229) | - | - |
| **Salio la mwisho wa 31 Disemba 2022** | **40,000** | **-** | **(32,537)** | **-** | **-** | **7,463** |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI

Faida kabla ya kodi
237%
Juni 2023: TZS 1,085 Milioni
Juni 2022: TZS 322 Milioni

Uwiano wa Faida (kabla ya kodi) na fedha za wanahisa
168%
Juni 2023: 25.71%
Juni 2022: 9.59%

Mapato ya riba
27%
Juni 2023: TZS 12,006 Milioni
Juni 2022: TZS 9,420 Milioni

## WARAKA MIZANIA

Mikopo
20%
Juni 2023: TZS 52,875 Milioni
Juni 2022: TZS 44,204 Milioni

Amana za wateja
20%
Juni 2023: TZS 57,130 Milioni
Juni 2022: TZS 47,620 Milioni

Mali
16%
Juni 2023: TZS 75,455 Milioni
Juni 2022: TZS 65,238 Milioni

Fedha za wanahisa
26%
Juni 2023: TZS 8,441 Milioni
Juni 2022: TZS 6,714 Milioni

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2023

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | (Kiasi kwa shilingi milioni) | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Robo ya Mwaka sasa 30 JUNI 2023 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30 JUNI 2022 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30 JUNI 2023 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30 JUNI 2022 |
| 1 Mapato ya Riba | 6,134 | 4,885 | 12,006 | 9,421 |
| 2 Gharama za Riba | (1,185) | (797) | (2,384) | (1,453) |
| 3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | 4,949 | 4,088 | 9,622 | 7,968 |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | 0 | - | 0 |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (310) | (660) | (775) | (1,270) |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,125** | **1,063** | **2,392** | **1,991** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 33 | 11 | 58 | 24 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 368 | 361 | 719 | 634 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 725 | 691 | 1,615 | 1,332 |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **(5,251)** | **(3,955)** | **(10,149)** | **(8,366)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (3,085) | (2,667) | (6,232) | (5,374) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | (145) | (137) | (274) | (267) |
| 7.3 Gharama Nyingine | (2,022) | (1,152) | (3,642) | (2,725) |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **513** | **535** | **1,085** | **322** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 65 | (24) | (107) | (24) |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **578** | **511** | **978** | **298** |
| 11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| **12 Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **578** | **511** | **978** | **298** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 392 | 401 | 392 | 401 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 58 | 51 | 49 | 15 |
| 15 Idadi ya Matawi | 8 | 8 | 8 | 8 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 3.1% | 3.2% | 2.7% | 1.0% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 28% | 31.8% | 25% | 9.4% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 72.3% | 66.5% | 70.5% | 73.3% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 37.9% | 38.5% | 38.0% | 39.1% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2023

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | (Kiasi kwa shilingi milioni) | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Robo Mwaka ya sasa 30 JUNI 2023 | Robo Mwaka iliyopita 31 MACHI 2023 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30 JUNI 2023 | Limbikizo la robo Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30 JUNI 2022 |
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 513 | 572 | 1,085 | 322 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 737 | 894 | 1,631 | 1,808 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (2,751) | (3,352) | (6,104) | (6,952) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 2,716 | 1,686 | 4,402 | 5,190 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (266) | 137 | (129) | (749) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 610 | (366) | 244 | (45) |
| - Kodi Iliyolipwa | (390) | (75) | (465) | (146) |
| - Mengineyo (bainisha) | (86) | (58) | (145) | (271) |
| *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **1,082** | **(563)** | **520** | **(842)** |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (157) | (43) | (200) | (81) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 6 | - | 6 | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato ahirishwa | (2) | (17) | (20) | (34) |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(153)** | **(60)** | **(214)** | **(116)** |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | (302) | (225) | (527) | - |
| Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | **(302)** | **(225)** | **(527)** | **-** |
| | | | - | - |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **627** | **(848)** | **(221)** | **(958)** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Kipindi | **9,429** | **10,277** | **10,277** | **9,575** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Kipindi | **10,056** | **9,429** | **10,056** | **8,618** |

## BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2023

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.

Imesainiwa na: Julius J Ruwaichi | Imesainiwa | Mtendaji Mkuu | Tarehe: 24 Julai 2023

Imesainiwa na: Tajinder Singh | Imesainiwa | Mkuu wa Idara ya Fedha | Tarehe: 24 Julai 2023

Imesainiwa na: Catherine Temu | Imesainiwa | Mkaguzi Mkuu wa Ndani | Tarehe: 24 Julai 2023

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2016, na zinaonyesha hali halisi.

Imesainiwa na: Thomas Engelhardt | Imesainiwa | Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi | Tarehe: 24 Julai 2023

Imesainiwa na: Johannes Mainhard | Imesainiwa | Mkurugenzi | Tarehe: 24 Julai 2023



Access Microfinance Bank Tanzania

# ACCESS MICROFINANCE BANK TANZANIA LIMITED
# MINIMUM DISCLOSURES OF BANK CHARGES AND FEES

| DESCRIPTION | CHARGE/FEE | |
|---|---|---|
| **ACCESS RAHISI,NORMAL SAVINGS, RAHISI CAA, ELIMU, AND KIKUNDI ACCOUNT(RAHISI ACCOUNT)** | **TZS** | **USD** |
| Required minimum opening balance | 10,000.00 | – |
| Monthly service fees | 2,000.00 | – |
| Cash withdrawal over counter up to 10M | 3,000.00 | – |
| Cash withdrawal over counter >10M | 10,000 | – |
| Bank statement 1free per month | FREE | – |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | – |
| New ATM card issuance | 10,000.00 | – |
| ATM card renewal or replacement | 15,000.00 | – |
| Replacement of the PIN | 10,000.00 | – |
| Standing order Internal | 2,000.00 | – |
| Standing order External | 12,980.00 | – |
| Dormant account fee | FREE | – |
| Interbank transfer | 10,000.00 | – |
| International transfer | $ 55 | 55.00 |
| Closure of account | 20,000.00 | – |
| **NUFAIKA TRANSACTIONAL ACCOUNT** | | |
| Required minimum opening balance | 50,000.00 | 25.00 |
| Monthly service fees | 6,000.00 | 3.00 |
| Bank statement 1free per month | FREE | FREE |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | 10.00 |
| New ATM card issuance | 15,000.00 | N/A |
| Fees per ATM withdrawal | 2,000.00 | N/A |
| Interbank transfer | 10,000.00 | 4.20 |
| International transfer | $ 55 | 55.00 |
| ATM mini statement | 1,000.00 | N/A |
| Standing order Internal | 2,000.00 | 1.00 |
| Standing order External | 12,980.00 | 12.98 |
| Dormant account fee | FREE | FREE |
| Reactivation of Dormant account | FREE | FREE |
| Letter of recommendation and certificate of balance | 50,000.00 | 23.00 |
| **NORMAL CURRENT ACCOUNT (NUFAIKA ACCOUNTS)** | **TZS** | **USD/EURO** |
| Required minimum opening balance | 100,000.00 | 50.00 |
| Monthly service fees | 6,000.00 | 3.00 |
| Cash withdrawal over counter up to 10M | 3,000.00 | 0.18% |
| Cash withdrawal over counter >10M | 10,000 | 10 |
| Fees per ATM withdrawal | 2,000.00 | N/A |
| ATM mini statement | 1,000.00 | N/A |
| Bank statement 1free per month | FREE | FREE |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | 10.00 |
| Cheque book 25 leaves | 20,000.00 | 10.00 |
| Cheque book 50 leaves | 35,000.00 | 15.00 |
| Dishonored cheque | 30,000.00 | 30.00 |
| Bankers Cheque | 50,000.00 | FREE |
| Stop payment | 30,000.00 | 30.00 |
| Standing order Internal | 2,000.00 | 1.00 |
| Standing order External | 12,980.00 | 12.98 |
| Balance enquiry | 1,000.00 | 1.00 |
| New ATM card issuance | 15,000.00 | N/A |
| ATM card renewal or replacement | 15,000.00 | N/A |
| Interbank transfer | 10,000.00 | 4.20 |
| International transfer | $ 55 | 55.00 |
| Dormant account fee | FREE | FREE |
| Reactivation of Dormant account | FREE | FREE |
| Letter of recommendation and certificate of balance | 50,000.00 | 23.00 |
| **SPECIAL ACCESS NUFAIKA ACCOUNT** | **TZS** | **USD/EURO** |
| Required minimum opening balance | 100,000.00 | 50.00 |
| Monthly service fees | 60,000.00 | 50.00 |
| Minimum monthly turover | 20,000,000.00 | 10,000.00 |
| Cash withdrawal over counter | FREE | 0.18% |
| Fees per ATM withdrawal | 2,000.00 | N/A |
| ATM mini statement | 1,000.00 | N/A |
| Bank statement 1free per month | FREE | FREE |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | 10.00 |
| Cheque book 25 leaves | 20,000.00 | 10.00 |
| Cheque book 50 leaves | 35,000.00 | 15.00 |
| Dishonored cheque | 30,000.00 | 30.00 |
| Bankers Cheque | 50,000.00 | FREE |
| Stop payment | 30,000.00 | 30.00 |
| Standing order Internal | 2,000.00 | 1.00 |
| Standing order External | 12,980.00 | 12.98 |
| Balance enquiry | 1,000.00 | 1.00 |
| New ATM card issuance | 15,000.00 | N/A |
| ATM card renewal or replacement | 15,000.00 | N/A |
| Interbank transfer | FREE | FREE |
| International transfer | $ 55 | 55.00 |
| Dormant account fee | 5,000.00 | 5.00 |
| Reactivation of Dormant account | FREE | FREE |
| Letter of recommendation and certificate of balance | 50,000.00 | 23.00 |
| **MIKAKATI SAVING ACCOUNTS** | **TZS** | **USD/EURO** |
| Required minimum opening balance | 20,000.00 | 20.00 |
| monthly service fees | FREE | FREE |
| Bank statement 1free per month | FREE | FREE |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | 10.00 |
| Cash withdrawal over counter | 1 FREE PER MONTH | 1 FREE PER MONTH |
| Subsequent Cash withdrawal over counter | 20,000.00 | 20.00 |
| Dormant account fee | FREE | FREE |
| International transfer | $ 55 | 55.00 |
| Account closure | 12,000.00 | 5.00 |
| **MIKAKATI PLUS SAVING ACCOUNTS** | **TZS** | **USD/EURO** |
| Required minimum opening balance | 10,000.00 | |
| monthly service fees | FREE | |
| Bank statement 1free per month | FREE | |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | |
| Cash withdrawal over counter | 1 FREE PER MONTH | |
| Subsequent Cash withdrawal over counter | 5,000.00 | |
| Dormant account fee | FREE | |
| International transfer | $ 55 | 55.00 |
| Account closure | 12,000.00 | |
| **KIKUNDI SAVING ACCOUNT** | **TZS** | |
| Required minimum opening balance | 10,000.00 | |
| monthly service fees | FREE | |
| Bank statement 1free per month | FREE | |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | |
| Cash withdrawal over counter | 3,000.00 | |
| Subsequent Cash withdrawal over counter | 3,000 | |
| Dormant account fee | FREE | |
| International transfer | $ 55 | |
| Account closure | FREE | |
| **BARAKA JUNIOR ACCOUNT** | **TZS** | **USD/EURO** |
| Required minimum opening balance | – | – |
| monthly service fees | FREE | FREE |
| Bank statement 1free per month | FREE | FREE |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | 10.00 |
| Cash withdrawal over counter | FREE | FREE |
| Subsequent Cash withdrawal over counter | FREE | FREE |
| Dormant account fee | FREE | FREE |
| International transfer | $ 55 | 55.00 |
| Account closure | FREE | FREE |

| | | |
|---|---|---|
| **TERM DEPOSIT RATES 2023** | | |
| **Amount** | | |
| 5,000,000 – 500,000,000 | | |
| > 500,000,000 | | |
| **AGENCY BANKING** | **To Govt** | **Old Customer Fee** |
| **Withdrawal (TZS) (agents) Range** | **TZS** | |
| 1 – 2,999 | 10 | 710 |
| 3,000 – 3,999 | 14 | 711 |
| 4,000 – 4,999 | 27 | 719 |
| 5,000 – 6,999 | 54 | 739 |
| 7,000 – 9,999 | 56 | 770 |
| 10,000 – 14,999 | 102 | 788 |
| 15,000 – 19,999 | 195 | 924 |
| 20,000 – 20,000 | 306 | 1,127 |
| 20,001 – 29,999 | 306 | 1,372 |
| 30,000 – 39,999 | 351 | 2,672 |
| 40,000 – 49,999 | 419 | 2,770 |
| 50,000 – 99,999 | 573 | 3,050 |
| 100,000 – 100,000 | 707 | 3,435 |
| 100,001 – 199,999 | 707 | 3,771 |
| 200,000 – 200,000 | 821 | 5,271 |
| 200,001 – 299,999 | 821 | 5,558 |
| 300,000 – 300,000 | 838 | 6,558 |
| 300,001 – 399,999 | 838 | 6,950 |
| 400,000 – 499,999 | 982 | 7,950 |
| 500,000 – 599,999 | 1,245 | 8,370 |
| 600,000 – 699,999 | 1,532 | 9,140 |
| 700,000 – 750,000 | 1,700 | 9,980 |
| 750,001 – 799,999 | 1,700 | 10,470 |
| 800,000 – 899,999 | 1,500 | 11,970 |
| 900,000 – 1,000,000 | 1,776 | 12,264 |
| 1,000,0001 – 3,000,000 | 1,875 | 13,230 |
| 3,000,0001 – 5,000,000 | 2,000 | 13,580 |
| **Deposit (TZS) (agents) Range** | **To Agent** | |
| 0 – 10,000 | 100 | |
| 10,001 – 20,000 | 150 | |
| 20,001 – 50,000 | 200 | |
| 50,001 – 100,000 | 350 | |
| 100,001 – 150,000 | 550 | |
| 150,001 – 200,000 | 700 | |
| 200,001 – 250,000 | 850 | |
| 250,001 – 300,000 | 900 | |
| 300,001 – 500,000 | 1,100 | |
| 500,001 – 750,000 | 1,200 | |
| 750,001 – 3,000,000 | 1,600 | |
| **MOBILE BANKING** | | |
| **Withdrawal – Bank to Wallet (TZS)** | **To Govt** | **Old Customer Fee** |
| 100–2,999 | 10 | 500 |
| 3,000–3,999 | 14 | 500 |
| 4,000–4,999 | 27 | 500 |
| 5,000–6,999 | 54 | 500 |
| 7,000–9,999 | 56 | 500 |
| 10,000–14,999 | 102 | 500 |
| 15,000–19,999 | 195 | 500 |
| 20,000–29,999 | 306 | 500 |
| 30,000–39,999 | 351 | 500 |
| 40,000–49,999 | 419 | 500 |
| 50,000–50,000 | 573 | 500 |
| 50,001–99,999 | 573 | 1,000 |
| 100,000–100,000 | 707 | 1,000 |
| 100,000–199,999 | 707 | 2,000 |
| 200,000–250,000 | 821 | 2,000 |
| 250,001–299,999 | 821 | 3,000 |
| 300,000–399,999 | 838 | 3,000 |
| 400,000–499,999 | 982 | 3,000 |
| 500,000–599,999 | 1,245 | 3,000 |
| 600,000–699,999 | 1,532 | 3,000 |
| 700,000–750,000 | 1,700 | 3,000 |
| 750,001–799,999 | 1,700 | 4,000 |
| 800,000–899,999 | 1,500 | 4,000 |
| 900,000–1,000,000 | 1,776 | 4,000 |
| 1,000,001–3,000,000 | 1,875 | 4,000 |
| 3,000,001–5,000,000 | 2,000 | 4,000 |
| **Deposit (TZS) (Wallet to Bank)** | **To Govt** | **Old Customer Fee** |
| 0 – 50,000 | – | FREE |
| 50,001 – 100,000 | – | FREE |
| 100,001 – 250,000 | – | FREE |
| 250,001 – 750,000 | – | FREE |
| 750,001 – 3,000,000 | – | FREE |
| **Air-time top-up** | – | FREE |
| **Utility payments** | – | FREE |
| **Balance inquiry** | – | 100 |
| **Mini-statement** | – | 200 |
| **Full account statement request** | – | 500 |
| **Cheque book request** | – | 600 |
| **AMBT internal transfers (same account holder)** | **Old Customer Fee** | **To AMBT** |
| 1 – 999 | – | FREE |
| 1,000 – 1,999 | 10 | FREE |
| 2,000 – 2,999 | 11 | FREE |
| 3,000 – 3,999 | 19 | FREE |
| 4,000 – 4,999 | 39 | FREE |
| 5,000 – 6,999 | 70 | FREE |
| 7,000 – 9,999 | 88 | FREE |
| 10,000 – 14,999 | 224 | FREE |
| 15,000 – 19,999 | 427 | FREE |
| 20,000 – 29,999 | 672 | FREE |
| 30,000 – 39,999 | 770 | FREE |
| 40,000 – 49,999 | 1,050 | FREE |
| 50,000 – 99,999 | 1,435 | FREE |
| 100,000 – 199,999 | 1,771 | FREE |
| 200,000, 299,999 | 2,058 | FREE |
| 300,000 – 399,999 | 2,450 | FREE |
| 400,000 – 499,999 | 2,870 | FREE |
| 500,000 – 599,999 | 3,640 | FREE |
| 600,000 – 699,999 | 4,480 | FREE |
| 700,000 – 799,999 | 4,970 | FREE |
| 800,000 – 899,999 | 5,264 | FREE |
| 900,000 – 1,000,000 | 6,230 | FREE |
| 1,000,001 – 3,000,000 | 6,580 | FREE |
| **AMBT internal outgoing transfers (other account holder)** | **To Govt** | **Old Customer Fee** |
| 1 – 2,999 | 10 | 510 |
| 3,000 – 3,999 | 14 | 511 |
| 4,000 – 4,999 | 27 | 519 |
| 5,000 – 6,999 | 54 | 539 |
| 7,000 – 9,999 | 56 | 570 |
| 10,000 – 14,999 | 102 | 588 |
| 15,000 – 19,999 | 195 | 724 |
| 20,000 – 29,999 | 306 | 927 |
| 30,000 – 39,999 | 351 | 1,172 |
| 40,000 – 49,999 | 419 | 1,270 |
| 50,000 – 99,999 | 573 | 1,550 |
| 100,000 – 199,999 | 707 | 1,935 |
| 200,000 – 299,999 | 821 | 2,271 |
| 300,000 – 399,999 | 838 | 2,558 |
| 400,000 – 499,999 | 982 | 2,950 |
| 500,000 – 599,999 | 1,245 | 3,370 |
| 600,000 – 699,999 | 1,532 | 4,140 |
| 700,000 – 799,999 | 1,700 | 4,980 |
| 800,000 – 899,999 | 1,500 | 5,470 |
| 900,000 – 1,000,000 | 1,776 | 5,764 |
| 1,000,001 – 3,000,000 | 1,875 | 6,730 |
| 3,000,001 – 5,000,000 | 2,000 | 7,080 |
| **FOREIGN EXCHANGE TRANSACTION** | **TZS** | **USD** |
| Telegraphic Transfer – Normal Customer (SWIFT) | 55.00 | 55.00 |
| TISS- Normal Customer | 10,000.00 | 4.20 |
| TISS-Staff | 6,000.00 | 2.10 |
| **LOAN PRODUCT LENDING RATES** | **TZS** | **USD** |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | from 66% to 72% | N/A |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 35,000,000 | from 46.8% to 60% | N/A |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 35,000,000 | om 49.2% to 74.4% | N/A |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 200,000,000 | om 26.4% to 33.6% | N/A |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | 20.40% | N/A |
| **Loan Processing Fee** | **TZS** | **USD** |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | 3.40% | N/A |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 50,000,000 | 3.40% | N/A |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 50,000,000 | 3.70% | N/A |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 200,000,000 | 2.90% | N/A |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | 1.50% | N/A |
| **Application Fee** | **TZS** | **USD** |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | 20,000.00 | N/A |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 50,000,000 | 20,000.00 | N/A |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 50,000,000 | 20,000.00 | N/A |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 200,000,000 | 20,000.00 | N/A |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | 20,000.00 | N/A |
| **Insurance Fee** | **TZS** | **USD** |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | 1.5% | N/A |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 50,000,000 | 1.5% | N/A |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 50,000,000 | 2.0% | N/A |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 150,000,000 | 1.5% | N/A |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | 1.5% | N/A |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hawa wa 'tuma kwa namba hii' bado tatizo

**MAMLAKA** ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imezuia vifaa vya mawasiliano pamoja na simu jumla vikiwa 108,395 kupokea na kutoa mawasiliano katika kipindi cha mwaka mmoja, kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo kujihusisha na uhalifu, ulaghai, vitendo vya udanganyifu na kuibiwa.

TCRA imebaini simu za ulaghai zinazoingia hapa nchini na hatua stahiki zimekuwa zikichukuliwa.

Kwa mujibu wa Mamlaka hiyo idadi ya simu za udanganyifu imeendelea kupungua kuanzia mwaka 2020 hadi Juni 2023. Lakini Septemba, mwaka jana, ilibaini matukio machache ya simu za ulaghai.

Pamoja na Mamlaka kuzuia vifaa hivyo, lakini tatizo la matapeli wa wizi wa mtandao wa simu, limeendelea na wananchi wanaibiwa pesa zao kwa mtindo wa 'hiyo hela tuma kwa namba hii'.

Kuna haja ya kampuni za simu kuangalia kwa makini vijana wanaowatumia kutoa huduma kwa wateja kwa sababu wengi wao hufanya kwa kipindi cha muda fulani na baadaye huondoka na wengi wao huwa wanafahamu mbinu za kuhamisha miamala au kushirikiana na matapeli kuwaibia wateja.

Baadhi ya matapeli hao huwapigia simu wateja wa mitandao ya kampuni za simu wanayotumia na kujifanya ni watoa huduma wanaotaka kuboresha huduma za simu zao.

Matapeli hao hufanya hivyo baada ya kugundua mteja ana kiwango cha kutosha cha muamala na kama mteja asipokuwa makini kugundua kuwa huyo anayempigia ni tapeli, anajikuta hela yake yote kwenye simu imekombwa.

Tunasema wizi wa mtandao unafanyika kwa kushirikiana na wafanyakazi wa kampuni hizo za simu kutokana na mbinu wanayotambua kuwa mteja ana kiwango fulani kwenye simu yake na humwibia kwa ujanja wanao ujua.

Kwa mfano hutumia mbinu ya kutuma ujumbe kuonyesha umepokea pesa halafu baada ya sekunde wanakupigia kukwambia muamala uliopokea umetumiwa kimakosa na kukutumia namba ya kuurudisha.

Mtu asipokuwa makini akifuata maelekezo ya kurudisha anakuwa anatumia pesa yake mwenyewe kuwatumia matapeli.

Jeshi la Polisi limekuwa likitoa taarifa kila mara kupitia ujumbe mfupi kwenye simu kuwatahadharisha wananchi kutokubali kuongea na mtu anayejifanya mtoa huduma wa kampuni ya simu kama namba anayopigiwa siyo 100 ambayo hutumiwa na kampuni za simu kama namba ya huduma kwa mteja.

Tunapongeza hatua iliyochukuliwa na TCRA ya kuzuia vifaa walivyobaini kutumika kwa ulaghai na tunaomba kampuni za simu zishughulikie tatizo hili la utapeli wa pesa kwa njia ya mtandao.

Matapeli wanapofanikiwa kuwaibia wateja pesa, hutoa laini za simu zao ili usiweze kuwafuatilia.


Swali linaloulizwa na wengi ni vipi watu wanapata usajili kiholela na mtu anayetapeli kushindwa kukamatwa.

Kampuni za simu zinaposajili laini za simu mtu anatakiwa awe na kitambulisho kinachotambulika ambacho ni cha taifa, ili anapofanya kosa iwe rahisi kukamatwa.

Lakini pamoja na juhudi zote hizo, utapeli wa njia ya mtandao unaendelea na watu kila kukicha wanalizwa.

Ni muhimu pia kwa wananchi kuwa makini na kuangalia namba wanazopigiwa kama zinatoka kwenye kampuni za simu kwa sababu zinatambulika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Taka miferejini kero, ziondolewe

Na Halfani Chusi

**WAHENGA** wana msemo wa kuwaonya wasiojali wala kufikiria mambo mema usemao, utavuna ulichokipanda, wakiutafsiri kwamba ukifanya jambo baya au uovu utavuna ubaya na ukiwekeza kwenye mambo mema utavuna mazuri.

Kwenye mifereji, inayopitisha majitaka kuna jambo baya linafanyika ambalo si rafiki kwa ustawi wa afya zetu na za mazingira.

Kumekuwapo na baadhi ya watu waliokosa umakini na upendo kwa mazingira na miundombinu wanatupa taka kwenye mifereji ya kupitisha maji taka hali ambayo husababisha maji kutofika sehemu lengwa lakini pia kuchochea uchafuzi wa hali ya hewa kwenye maeneo husika.

Janga la magonjwa ya mlipuko ni tatizo linaloitesa dunia kwa sasa, vivyo hivyo nchi yetu kwa sasa inapitia kwenye magonjwa mengi ya mlipuko ambayo chanzo chake ni uchafu hivyo kuna haja ya kuweka mkakati wa kuzuia utupaji wa taka kwenye mifereji.

Ukipita kwenye mifereji mingi unakuta imepambwa na taka hasa za plastiki kama chupa za maji, ambazo haziozi na kusababisha maji kutuama sehemu moja kwa muda mrefu na kutengeneza mazalio ya mbu, wadudu hasa funza, wanyama wakiwamo panya na vyura.

Kiafya majitaka yanapotuama sehemu moja kwa muda mrefu husababisha madhara mengi ikiwamo mazalia ya mbu, ambao husababisha malaria, harufu mbaya kwa kuwa hayatembei na wakati mwingine hupelekea kuchafua taswira ya eneo.

Ni vyema tukawa na tahadhari dhidi ya uhifadhi wa taka, ili kuzuia magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu ambacho chimbuko lake kubwa ni kula kinyesi cha mgonjwa wa maradhi hayo, pengine kupitia kwenye chakula, kinywaji au matunda.

Mataifa mengine yamefanikiwa kwenye eneo la utunzaji wa mazingira kwa kufunika mifereji na kuweka utaratibu bora wa kuzoa na kuhifadhi taka.

**Kwenye mifereji, inayopitisha majitaka kuna jambo baya linafanyika ambalo si rafiki kwa ustawi wa afya zetu na za mazingira.**

Lakini mbali na jitihada hizo pia, kuna hitajika usimamizi wa sheria kwa yule atakayekutwa ametupa taka kwenye mtaro. Imani yangu ni kwamba hili litasaidia kutunza na kuilinda mifereji yetu.

Ustawi wa nchi na muonekano mzuri unajengwa na ulinzi na uhifadhi wa mazingira yake, ikiwa ni pamoja na kutunza mifereji inayosafirisha maji taka kwenda sehemu mahususi kwa ajili ya kuhifadhi.

Lakini pia, kutotupa taka mahali ambako sio sahihi, ninashauri Tanzania kila baada ya kilomita kadhaa mfano tatu kuwe na pipa la taka kwaajili ya kuhifadhi takataka, hili itasaidia watu kutotupa taka ovyo na baadala yake watazihifadhi kwenye maeneo haya yaliyoandaliwa mahsusi.

Ni kwa muda mrefu katika pitapita zangu nimeshuhudia watu wakishawishika kutupa taka mahali pasipostahili kutokana na kukosekana kwa maeneo sahihi ya kuhifadhi au dampo kuwa mbali na sehemu waliko.

Wakati mwingine inaweza kuwa pipa la taka liko mbali, au halipo katika eneo fulani jambo la muhimu hapa nikuona namna gani mtu atapata urahisi wa kuhifadhi taka ili kuepukana na kishawishi cha kutupa mahali pasipo stahili.

Serikali imekuwa ikitoa maonyo dhidi ya utupaji wa taka ovyo lakini bado kumekuwa na ugumu wa watu katika kufuata utaratibu huo, lakini ukweli ni kwamba tunapaswa kubadilika wenyewe kila mmoja wetu kubadilika.

Kwa kufanya hivyo kutasaidia kufikia nchi safi, kila eneo hata mitaro itakuwa safi kwa sababu usafi unaanzia ndani ya mtu mwenyewe.

## Dereva bajaji mbaroni tuhuma za kuua mgambo kwa kumchoma kisu

**Na Mary Mosha,** MOSHI

JESHI la Polisi mkoani Kilimanjaro linamshikilia Abdan Abdi (24), dereva bajaji kwa tuhuma za kusababisha kifo cha Michael Ngulizi (55), askari wa Jeshi la Akiba (Mgambo), mkazi wa Majengo kwa Mtei, Manispaa ya Moshi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Simon Maigwa, alisema tukio hilo lilitokea Julai 21 mwaka huu saa sita mchana huko Majengo kwa Mchomba, Kata ya Majengo, wilayani Moshi ambako askari huyo alijeruhiwa kwa kitu chenye ncha kali ubavuni na mtuhumiwa huyo.

"Baada ya kujeruhiwa, alikimbizwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa (Mawenzi) ambako alifikwa na umauti wakati akiendelea na matibabu.

"Mtuhumiwa baada ya kutenda tukio hilo alikimbilia mkoani Tanga. Jeshi la Polisi kwa ushirikiano na raia wema, tuliendelea na msako na Julai 23 tulifanikiwa kumtia mbaroni.

"Uchunguzi wa awali unaonesha chanzo cha tukio hilo ni mtuhumiwa kujifungia ndani alipopata taarifa za kutafutwa na polisi baada ya kudaiwa kuwatishia kuwaua baadhi ya ndugu zake.

"Tulikuwa tunamtafuta kwa kosa la kuwatishia maisha ndugu zake na kufanya fujo. Ninawasihi wananchi kufuata sheria, kanuni na taratibu," alisema Kamanda Maigwa.

Mwanaidi Omari, shuhuda wa tukio hilo, alisema: "(Mtuhumiwa) alianza kumtishia kumuua baba yake wa kambo jana. Kwa jitihada tulitafuta msaada, tulikwenda polisi kuwaambia kuna mtu amemvamia baba yake mdogo anataka kumuua. Hawakufika kwa wakati.

"Kabla ya tukio hili Julai 20 mwaka huu alionekana kuingia ndani na vitu vyenye ncha kali pamoja na mawe akitishia kumuua baba yake wa kambo.

"Kutokana na polisi kutofika kwa wakati, uongozi wa mtaa ulimwagiza askari mgambo akamkamate mtuhumiwa. Katika purukshani hizo ndipo akachomwa kisu."

Mwenyekiti wa Mtaa kwa Mtei, Mary Kimei, alisema tukio hilo, lilitokea na kuacha majeraha makubwa kutokana na uchapakazi na umahiri wa askari huyo katika kusaidia jamii.

"Ifike mahali wazazi tujikite katika maadili ya watoto. Usimwone mtoto wako anatumia dawa za kulevya ukamchukulia poa, toa taarifa na hatua za kisheria zitachukuliwa. Viongozi wa dini wazidi kuhubiri.

"Jeshi la polisi lichukue hatua mara linapopewa taarifa hasa za watu kutishia maisha ili kuepusha mauaji," alisema.

**"Kabla ya tukio hili Julai 20 mwaka huu alionekana kuingia ndani na vitu vyenye ncha kali pamoja na mawe akitishia kumuua baba yake wa kambo.**



Kaimu Mkurugenzi wa jarida la KIKI, Alphonce Marealle (kushoto), akikata utepe kuzindua jarida hilo, jijini Dar es Salaam jana, linaloandaliwa na kampuni ya ABC Bros kwa udhamini wa Ubalozi wa Uholanzi, lenye lengo la kutoa elimu mbalimbali kwa vijana wa kitanzania kujitambua na kujikwamua kiuchumi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

RIPOTI YA HAKI JINAI

# LHRC yaibuka na hoja tano kwa serikali, taasisi na wadau

**Na Sabato Kasika**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimetoa mapendekezo matano kinayoamini yakifanyiwa kazi, yatasaidia utekelezaji wa haraka wa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai.

Katika mkutano na waandishi wa habari ofisini kwake jana, Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Dk. Anna Henga, alisema mapendekezo yao yanajumuisha vyombo vinavyohusika na haki jinai kuanza kutekeleza mapendekezo ya tume, hasa yale yasiyohitaji matumizi ya fedha au kubadilisha sheria.

"Hoja yetu ya pili ni kwamba, wadau wa haki jinai kwa kushirikiana na serikali, watoe elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kutii sheria bila shuruti ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima na vyombo vya dola," alisema Dk. Anna.

Alisema hoja yao ya tatu ni taasisi zinazoguswa na mapendekezo ya tume kuandaa mpangokazi juu ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyogusa taasisi zao.

Mkurugenzi huyo pia alipendekeza kuwapo mfumo wa kufanya tathmini ya utekelezaji wa hoja za tume na kati hoja yake ya tano, akaitaka serikali kupeleka muswada bungeni katika mkutano wa Septemba mwaka huu ili kurekebisha sheria zinazokwaza utekelezaji wa mapendekezo ya tume. Kuna mapendekezo yanahitaji mabadiliko ya sheria.

**ADHABU YA KIFO**

"Pamoja na hoja zetu hizo, pia kuna eneo lingine ambalo tumekuwa tunaishauri serikali ambalo ni adhabu ya kifo, kwamba ifutwe. Kwa mujibu wa tume, kifo ni adhabu katili inayotweza utu wa mtu na iko kinyume cha haki za binadamu.

Hivyo, inapaswa kutokuwa adhabu ya lazima. Ikitokea mtu amehukumiwa adhabu hiyo, ikapita miaka mitatu Rais hajaidhinisha kunyongwa, basi adhabu igeuke kuwa kifungo cha maisha," alisema.

Januari mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan aliunda Tume ya Haki Jinai, ikiongozwa Jaji Mkuu mstaafu, Othman Chande, kwa lengo la kuangalia namna kuboresha taasisi za haki jinai nchini.

Kwa mujibu wa hadidu za rejea, taasisi zilizotakiwa kufanyiwa kazi ni Jeshi la Polisi, Magereza, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) na Ofisi ya Mashtaka.

Julai 15, mwaka huu, tume hiyo iliwasilisha mapendekezo yake kwa Rais baada ya kufanya kazi kwa miezi sita.

**"Hoja yetu ya pili ni kwamba, wadau wa haki jinai kwa kushirikiana na serikali, watoe elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kutii sheria bila shuruti ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima na vyombo vya dola," alisema Dk. Anna.**

**KABWELA** FADHILI MOHAMED



HABARI KITAIFA

# Mtuhumiwa dawa za kulevya aachiwa huru

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi imemwachia huru Bahati Melitano baada ya upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha kosa la kusafirisha dawa za kulevya lililokuwa linamkabili.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi mbele ya Jaji Immaculata Banzi baada ya kumaliza kusikiliza shauri hilo katika Masjala ndogo ya Bukoba.

Inadaiwa kuwa Aprili 23, 2022, katika Kijiji cha Mtundu wilayani Biharamulo mkoani Kagera, Bahati alijihusisha na biashara haramu ya kusafirisha dawa za kulevya.

Mshtakiwa anadaiwa kukutwa na kilo 199.9 za dawa hizo aina ya bangi. Aliposomewa mashtaka alikana kutenda kosa hilo.

Upande wa Jamhuri uliwakilishwa na jopo la mawakili wa serikali; Tully Helela, Erick Mabagala, Mgeni Mdee, Matilda Assey, Glory Lugeye na Agnes Awino.

Upande huo wa Jamhuri uliita mashahidi wanane na vielelezo saba ambapo katika ushahidi wao, shahidi wa kwanza, F5034 Sajenti Ignas anadai akiwa na wenzake katika doria siku ya tukio walipata taarifa kutoka kwa msiri kuwa nyumbani kwa Bahati kulikuwa na bangi.

Inadaiwa waliandaa hati ya upekuzi, walifika kufanya upekuzi katika nyumba hiyo na kufanikiwa kukuta viroba 10 vyenye majani yaliyodhaniwa kuwa bangi. Walimkamata mtuhumiwa na kumfikisha kituo cha polisi kisha mahakamani.

Katika utetezi wake, Bahati alidai Aprili 23, 2022, alipokuwa nyumbani kwake kalala na mke wake na mtoto, saa sita usiku alisikia mlango ukigongwa na watu waliojitambulisha wenyewe kama maofisa wa polisi.

Baada ya kufungua mlango, aliona askari polisi watatu na mgambo mmoja ambaye alimfunga pingu na kumweka chini ya kizuizi.

Mshtakiwa anadai alionyeshwa viroba vilivyokuwa nje ya nyumba yake, aliona pia gari limeegeshwa umbali wa takribani hatua 20 hadi 25 kutoka nyumbani kwake.

Anadai baada ya hapo, mwenyekiti wa eneo aliitwa, alipofika aliwaita majirani, walipekua nyumba yake kuanzia sebuleni hadi chumbani, lakini hawakupata chochote.

Mshtakiwa anadai baada ya upekuzi, watu wengine walitia saini katika hati lakini yeye hakutia saini.

Anadai kuwa baada ya maofisa hao kutia saini, majirani na mgambo waliamriwa kupandisha mifuko katika gari kisha akapelekwa Kituo cha Polisi Nyakanazi.

Mahakama baada ya kusikiliza ushahidi huo, iliona upekuzi ulifanyika isivyo halali na kutokana na upekuzi huo batili, upande wa Jamhuri umewasilisha ushahidi usio na uzito.

"Kwa kukosekana kwa kielelezo namba 1, 2 na 6, hakuna ushahidi wowote wa kumwunganisha mshtakiwa na kosa linalodaiwa kwa kuzingatia ukweli kwamba mtuhumiwa alikana kukutwa na kielelezo namba mbili ambacho ni bangi.

"Baada ya kusikiliza pande zote, mahakama inaona upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha kesi dhidi ya mshtakiwa bila kuacha shaka, hivyo mshtakiwa Bahati Melitano anaachiwa huru hana hatia," alisema Jaji Banzi.



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, Mohamed Moyo (mwenye kofia), akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Naipanga juzi na kumwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Mhandisi Chionda Kawawa (kulia), kuhakikisha yanajengwa madarasa mawili ya Shule ya Msingi Naipanga, ili kuwaondolea adha wanafunzi ukosefu wa majengo ya kusoma. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Bodaboda adaiwa kumjeruhi kwa mapanga mwanafunzi

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MWANAFUNZI wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Uduru wilayani Hai mkoani Kilimanjaro (jina tunalo) amecharangwa mapanga na dereva pikipiki (bodaboda) kwa tuhuma za kumpa simu mdogo wa bodaboda huyo iliyosababisha kutofanya vizuri katika masomo yake.

Mwanafunzi huyo alimweleza mwandishi wa habari hizi kuwa Julai 17 mwaka huu asubuhi, wakati anakwenda shuleni, alikutana na dereva huyo ambaye alichomoa panga na kuanza kumshambulia maeneo mbalimbali ya mwili ikiwamo kichwa, miguuni na mikononi.

"Ilikuwa asubuhi ninaelekea shuleni, nilikutana na bodaboda huyo, nikamsalimia hakuitikia. Ghafla alichomoa panga kiunoni na kuanza kunishambulia huku akinituhumu nimempa mdogo wake simu janja anayoitumia kuwasiliana na wanaume badala ya kusoma, jambo ambalo si kweli.

"Nilianza kupiga kelele katika kuomba msaada ndipo walipotokea wazee wawili wakaniokoa na baada ya hapo sikujua kilichoendelea hadi nilipojikuta nipo hospitalini daktari ananisafisha vidonda na kunifunga vitambaa vyeupe," alisema.

Baadhi ya mashuhuda, akiwamo Tumaini Tumsifu, walidai kuwa asubuhi siku hiyo, walisikia kelele za kuomba msaada ndipo walipotoka na kukutana na kijana huyo akiwa na panga lenye damu huku akitoa lugha za matusi.

Mwenyekiti wa kitongoji hicho lilikofanyika tukio hilo, Peter Masawe, alithibitisha binti huyo kutendwa ukatili huo na kijana huyo aliyemtaja ni Hilary Mafue, dereva bodaboda na alikimbizwa katika zahanati kupatiwa matibabu.

"Nilikwenda hadi zahanati ambako nilimkuta anapatiwa matibabu, kisha nikaenda polisi na kutoa taarifa tena. Kabla sijaenda niliwasiliana na mwenyekiti wa kijiji na kumpa taarifa, tukaongozana kwenda shuleni ambako tulikuta tayari wameshapata taarifa juu ya tukio.

"Bado ni tatizo kubwa kwenye matukio ya aina hii maana hata tunapochukua hatua ya kuwakamata na kuwapeleka kituoni baada ya muda wanaachiwa," alililalamika Masawe:

# CHAVITA yalia wenye ulemavu kutoshirikishwa katika vyombo vya uamuzi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

BAADHI ya vyombo vya uamuzi kuanzia ngazi ya mtaa, vinaelezwa kutoshirikisha kundi la watu wenye ulemavu na hivyo kuwakosesha haki ya kufikisha mawazo yao katika shughuli mbalimbali.

Kutokuwa na uwakilishi katika vyombo hivyo pia kumetajwa kuwa moja ya sababu za kundi hilo kutofikisha kero zake ili zitafutiwe ufumbuzi na kuwafanya watekeleze majukumu yao sawa na wengine.

Kwa kutambua hilo Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA) Mkoa wa Pwani, kikaomba ufadhili kwa Shirika la The Foundation for Civil Society (FCS) ili kutoa elimu kwa makundi mbalimbali wakiwamo watendaji wa kata, viongozi wa vyama vya siasa na madiwani.

Mwenyekiti wa CHAVITA Mkoa wa Pwani ambaye ni mratibu wa mradi huo, Adam Shabani, alisema lengo ni kuhakikisha ujumuishaji wa watu wenye ulemavu katika vyombo vya uamuzi kuanzia ngazi ya mtaa.

Kwa mujibu wa Shabani, awamu ya kwanza ya mradi wa elimu hiyo matokeo hayakuwa mazuri ndipo wafadhili waliporidhia kutoa fedha kwa mara nyingine kwa ajili ya awamu ya pili ili jamii iwatambue na kuwajumuisha wenye ulemavu katika vyombo vya uamuzi.

Mradi huo unalenga kuona matokeo chanya katika kuongeza ushawishi kwa jamii kwa kuwa sehemu nyingi wamekuwa wakiacha kundi hilo kuwashirikisha mambo mbalimbali.

Akizungumza kwa niaba ya Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Pwani, Christopher Rusatila, alielekeza viongozi na wananchi kuanzia ngazi ya mitaa kuwashirikisha watu wenye ulemavu katika vyombo vya uamuzi.

"Kutosikia au kuwa na ulemavu wowote ule sio ugonjwa. Hawa watu wanaweza kuwa wabunifu kama walivyo wengine, tuwakubali na kuwajumuisha katika nafasi mbalimbali," alisema.

Tatu Kondo, Mjumbe wa Chavita Mkoa wa Pwani, alimweleza mwandishi kwamba kundi hilo likishirikishwa katika ngazi za uamuzi litawatetea wengine na kufikisha mahitaji yake kunakotakiwa kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi.

Kondo alisema jamii inatakiwa kuamini kwamba wenye ulemavu wana uwezo sawa na wengine, hivyo hata uchaguzi ujao wapewe nafasi kuanzia ngazi za mitaa hadi kitaifa.

Mkataba wa haki za watu wanaoishi na ulemavu ulianza kutekelezwa nchini Desemba 13, 2006, unaelekeza kundi hilo kupewa haki sawa kama raia wa kawaida.



## Watuhumiwa 106 wafikishwa kortini kwa makosa ya uhalifu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Arusha limesema kwa kipindi cha Januari hadi Juni mwaka huu limewafikisha mahakamani watuhumiwa wa makosa makubwa ya uhalifu mbalimbali, kwamba 106 walipatikana na hatia na kuhukumiwa kwenda jela.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, aliyasema hayo jana jijini hapa na kueleza kuwa watuhumiwa hao walihukumiwa baada ya kupatikana na makosa ya ubakaji, ulawiti, kusafirisha dawa za kulevya, unyang'anyi wa kutumia silaha, mauaji na kupatikana na nyara za serikali.

Kamanda Masejo alisema kati ya watuhumiwa hao 25, walihukumiwa vifungo vya maisha jela kwa makosa ya ubakaji, ulawiti na mauaji.

"Watuhumiwa 30 walihukumiwa kwenda jela miaka 30 kwa makosa ya unyang'anyi wa kutumia silaha na kusafirisha dawa za kulevya, ambapo watano walihukumiwa vifungo vya miaka 20 kwa makosa ya kupatikana na nyara za serikali," alisema.

Alisema Jeshi la Polisi pia limefanikiwa kupunguza matukio ya uhalifu mkoani Arusha kwa asilimia 11 kwa kuwa takwimu zinaonyesha kuanzia Januari hadi Juni mwaka 2022, makosa yalikuwa 1,345 hali ambayo ni tofauti na kipindi kama hicho mwaka huu,kwa kuwa makosa yaliyoripotiwa ni 1,198 sawa na upungufu wa makosa 147.

"Pia kwa kipindi kama hicho, tulifanikiwa kupunguza ajali za barabarani kwa asilimia 59 kwa mwaka 2022 ajali zilizoripotiwa zilikuwa 184 ukilinganisha na ajali 76 zilizotokea mwaka huu, ni sawa na upungufu wa ajali 108," alisema.

Alisema kupitia misako mbalimbali ambayo ilifanyika kuanzia Januari hadi Juni mwaka huu,dhidi ya dawa za kulevya walifanikiwa kukamata mirungi kilogramu 747 na gramu 695, bangi tani 2.5 na kuteketeza tani tano na hekari 60 za bangi, lakini pia walikamata heroine gramu 560.75.

Alisema kwa kipindi hicho walikamata watuhumiwa 233, wakiwa na pombe ya moshi maarufu kwa jina la gongo lita 1,091 pamoja na mitambo 21 ya kutengeneza pombe hiyo haramu.

"Jeshi letu la Polisi limeimarisha ulinzi maeneo yote hasa kwa kuzingatia kipindi hiki ambacho kuna ongezeko kubwa la watalii (high season) pamoja na uwepo wa mikutano mbalimbali ya kimataifa, ambayo inaendelea kufanyika katika mkoa wetu, likiwa ni kuitangaza sifa njema ya nchi yetu, ili kuvutia watalii wengi zaidi pamoja na utalii wa mkutano," alisema.

Hivyo, aliwaomba wananchi kuendelea kutoa taarifa dhidi ya vitendo vya uhalifu vinavyotokea katika maeneo yao, ikiwemo ukatili dhidi ya watoto pamoja na wanawake, ili wachukuliwe hatua za kisheria dhidi ya wote watakaobainika.

# Mawakala utalii watakiwa kuripoti mgeni mashuhuri anapozuru nchini

**Na Mary Mosha,** HAI

SERIKALI imesema kuna umuhimu kwa mawakala wa utalii nchini, kutoa ushirikiano wa taarifa za uwapo wa wageni mashuhuri duniani wanaokuja kutembelea hifadhi za taifa kupitia kampuni zao.

Imesema lengo ni kuweka nguvu ya pamoja kuitangaza nchi kimataifa pamoja na vivutio vilivyopo nchini.

Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk.Hassan Abbasi, aliyasema hayo jana wakati akiaga watu wanakwenda kupanda Mlima Kilimanjaro.

Watu hao wapatao 19 wanaongozwa na mpiga kinubi maarufu duniani, Siobhan Brady.

Brady ni raia wa Ireland pia ni mwanamuziki aliyeshinda tuzo za Guiness kwa kupiga kinubi katika milima ya Himalaya, kwa sasa anakusudia kuvunja rekodi hiyo kwa kupanda Mlima Kilimanjaro, kwenda kupiga kinubi katika kilele cha mlima huo.

Akizungumza katika hafla ya kuwaaga wapanda mlima hao, Dk.Abbasi.alisema wako watu wengi maarufu kutoka maeneo mbalimbali duniani wanaokuja Tanzania na wanaokuwa wa kwanza kufahamu hayo ni kampuni za utalii, hivyo ni vyema wakajenga utaratibu wa kuishirikisha serikali ili kuongeza kasi ya kuitangaza nchi kimataifa.

"Niombe wenzetu waratibu wa ziara mbalimbali za kitalii, kuna watu wengi mashuhuri kutoka duniani wanakuja Tanzania, kwa kuwa wa kwanza kufahamu ni kampuni za utalii wanaowaleta, ukimficha maana yake unaiharibia nchi yako. Tuko kwenye kipindi kikubwa cha kutangaza utalii wetu,tushirikiane kwa karibu ili kufanikisha hili.

"Mchezaji maarufu anakuja hutuambii lolote Watanzania mpaka anaondoka, akiamua kuweka kwenye mitandao ndio tunaona kumbe fulani alikuwa Tanzania siyo kitu chenye manufaa mema kwa nchi yetu. Niombe kampuni za utalii mnapopata wageni ambao wanaweza kutusaidia kutangaza nchi yetu tushirikishane," alisema.

Dk.Abbas alisema Brady akiweza kuvunja rekodi ya Guiness kwa kupiga kinubi katika kilele cha Mlima Kilimanjaro kutaweka rekodi kubwa duniani na kuitangaza Tanzania pamoja na vivutio vilivyopo kimataifa.

Naye Brady alisema wameamua kupanda Mlima Kilimanjaro ambao ni mrefu zaidi Afrika ili kushuhudia na kufurahia uzuri uliopo katika kilele cha mlima huo ambapo atapiga kinubi na kuivunja rekodi aliyoiweka awali.

Samira Mauly, mmoja wa wakurugenzi wa Kampuni ya Utalii ya Mauly Tours & Safaris, alisema kupata watu maarufu wanaofika kufanya utalii nchini kunapanua wigo wa kuutangaza utalii kimataifa.




Mkurugenzi wa Hazina wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Wenceslaus Fungamtama (katikati), akikata utepe kuzindua vyoo vyenye matundu 18 vilivyojengwa na benki hiyo, katika Shule ya Msingi Kikelelwa, wilayani Rombo mkoani Kilimanjaro mwishoni mwa wiki. Wengine ni Ofisa Elimu ya Msingi wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Alice Makule (wa tatu kulia) na (wa tatu kushoto) ni Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Charles Amos. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waliopigana vita Uganda watoa somo la uzalendo kwa vijana

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

BAADHI ya mashujaa walioshiriki katika vita ya Tanzania na Uganda wamewataka vijana nchini, kuwa wazalendo na kudumisha nidhamu, kwa ajili ya kuilinda amani ya nchi.

Wito huo umetolewa jana jijini Arusha na Luteni Kanali, Felix Ngatoni wakati wa maadhimisho ya kumbukumbu ya Siku ya Mashujaa nchini.

Luteni Kanali Felix alishiriki vita hiyo akiwa mmoja wa askari walioendesha kifaru cha kwanza katika Daraja la Kyaka lililoko mkoani Kagera.

Alisisitiza umuhimu wa vijana kulipenda taifa lao, kwa kuhakikisha amani waliyoipigania mashujaa inaendelea kudumishwa.

Alisema haikuwa rahisi kumdhibiti nduli Idd Amini, lakini kwa kuwa walikuwa wazalendo na watii wa nchi walifanikiwa kumdhibiti kwa kuangusha ndege ya adui na kusababisha arudi nyuma.

"Kupitia utii na uzalendo ambao ulituunganisha kama ndugu, tuliweza kufanya mengi ikiwemo kuchimba mahandaki kwa mikono, kuhifadhi watu na vifaa vya kazi kwa kuwa hali hii ikiendelezwa na vijana wa sasa amani ya nchi yetu haitatoweka," alisema.


Aidha,aliwasihi vijana kuishi kwa maadili ya kitanzania na kuachana na tabia za ughaibuni za kuvaa mavazi ya kuchanwa (suruali), dharau kwa wakubwa kwani siyo afya kwa ustawi wa taifa.

Mwenyekiti wa Muungano wa Wanajeshi Wastaafu, Sajenti Gabriel Hosea Bonda, aliiomba serikali kufahamu wastaafu wapo na walipigania amani ya nchi.

"Wastaafu tupo historia ya vita ya Kagera tunaijua sisi, utendaji tulioufanya kwa uzalendo kwa nchi hii, tuligangamala hadi adui akarudi nyuma,hivyo serikali ielewe na ijuwe wapiganaji wake tupo wapi na maisha yetu yapoje,kwa sababu hali zetu haziridhishi kama wastaafu na ni wajibu wao kuhakikisha tupo vizuri, " alisema.

Maadhimisho hayo yalihudhuriwa na Mkuu wa Mkoa Arusha, John Mongella, viongozi wa dini na watendaji wa serikali ambao waliweka dhana za jadi kwenye mnara wa kumbukumbu wa mashujaa.

Dhana hizo ni mkuki, ngao, mshale, shoka ambapo viongozi wa dini kwa pamoja waliweka mashada ya maua kama ishara ya kuwaenzi mashujaa hao.





# Ahadi ya Samia yatekelezwa Ngara

**Na Mwandishi Wetu,** NGARA

WANANCHI wa Wilaya ya Ngara mkoani Kagera, wameishukuru serikali kwa kutekeleza kwa haraka ahadi ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kutatua kero ya upatikanaji wa maji iliyokuwa ikiwakabili kwa kipindi kirefu.

Ni ahadi aliyoitoa akiwa wilayani hapa Februari 22, 2022 wakati wa sherehe za maadhimisho ya Askofu Severin Niwemugizi ya kutimiza miaka 25 katika jimbo la Rulenge Ngara.

Kutokana na kero hiyo, Rais Samia alimwagiza Waziri wa Maji, Jumaa Aweso kutatua tatizo hilo Ngara mjini.

Ikiwa takribani mwaka mmoja na nusu tangu atoe agizo hilo, tayari limetekelezwa kwa kujengwa mradi wenye thamani ya Sh. milioni 904 na kuzinduliwa juzi na Waziri Aweso aliyeambatana na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Nadhifa Kemikimba.

Akizungumza mara baada ya uzinduzi wa mradi huo, mmoja wa wananchi, John Ndaibise, alieleza kufurahishwa na utekelezaji wa agizo hilo baada ya kuhangaika na adha ya upatikani wa huduma hiyo kwa kipindi kirefu.

"Hakika wanawake wa Ngara wametuliwa ndoo vichwani maana walikuwa wakitumia muda mrefu kutafuta maji na wakati mwingine kushindwa kufanya shughuli zao za kimaendeleo. Sasa maji haya yatatusaidia kuinua shughuli zetu za kiuchumi," alisema.

Katika agizo lake Rais Samia alimtaka Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji kuelekeza fedha kubadili miundombinu ya usambazaji maji Ngara mjini na kuwapatia wahandisi wa maji wa eneo hilo gari ili kuimarisha utendaji kazi.

Akizindua mradi huo unaotarajia kuwahudumia zaidi ya wananchi 18,270, Aweso alimpongeza mkandarasi wa mradi huo kwa kutekeleza haraka bila kuwa na ubabaishaji.

Aidha, aliwataka wananchi kutunza miundombinu ya mradi huo ili uendelee kuwahudumia na kuinua uchumi wa wananchi.

Waziri Aweso anaendelea na ziara yake mkoani Kagera kwa lengo la kukagua utekelezaji wa miradi ya maji na kubaini changamoto mbalimbali za upatikanaji wa maji.



Waziri wa Maji, Jumaa Aweso (wa tatu kulia), akimsikiliza Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mhandisi Jumanne Magungu, akielezea kuhusu mradi wa maji wa Wilaya ya Ngara mkoani Kagera kabla ya kuuzindua juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi waomba kuendelea kuishi hifadhini

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI wa vijiji sita wilayani Shinyanga ambao wamevamia eneo la Hifadhi ya Msitu wa Nindo wilayani hapa, wamemwomba Rais Samia Suluhu Hassan waendelee kuishi kwenye hifadhi hiyo, kutokana na eneo walilomegewa kuwa finyu na tayari wanaishi watu.

Hifadhi ya Msitu wa Nindo ilitambuliwa kisheria na kutangazwa na gazeti la Serikali Namba 10 mwaka 1958, ikiwa na ukubwa wa hekta 27,446 lakini baada ya wananchi kuvamia na kuishi humo, eneo la hifadhi limesalia hekta 10,969 na serikali ikaona hekta 3,726 iwamegee wananchi ili waishi na hekta 7,243 zibaki kwa ajili ya hifadhi. Wakizungumza katika mkutano wa hadhara ambao ulikuwa na ajenda ya kumwomba Rais Samia awaache waendelee kuishi ndani ya hifadhi hiyo, wananchi hao walishukuru kwa kutengewa eneo licha ya kusema kuwa eneo hilo ni finyu.

Mmoja wa wananchi hao, Pete Buhemba, alisema wanamshukuru Rais Samia kwa kuwajali na kuwatengea eneo la makazi ndani ya hifadhi hiyo lakini eneo hilo haliwatoshi kwa kuwa tayari kuna watu wanaishi na wanamiliki mashamba.

Walisema hali hiyo inaweza kuzua hofu ya kuwapo migogoro ya ardhi na hata kukosa maeneo ya kufanya shughuli za kilimo.

Mwananchi mwingine, Sylvester Shimbolya, alisema eneo hilo lisingekuwa na wananchi wanaoishi lingewatosha na kuishi kwa amani kwa kuwa wangefanya shughuli za kilimo na ufugaji bila bughudha yoyote, lakini sasa hivi wanahofia usalama wao kwa sababu watakwenda kuishi katika maeneo ya watu wengine.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Lyamidati, Dotto Mende, alisema wananchi wa vijiji hivyo wako zaidi ya 1,000 na katika baadhi ya kaya, kuna watu kuanzia 10 hadi 30 na hofu yao kubwa ni kukosa maeneo ya kulima kutokana na kutegemea shughuli za kilimo.

Hivi karibuni Mhifadhi Mkuu Daraja la Pili kutoka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Kanda ya Magharibi, Lucas Nyambala, akiwa mkoani Shinyanga katika kikao cha kujadili utekelezaji wa uamuzi wa mawaziri wanane wa kisekta ya juu ya utatuzi wa mgogoro wa hifadhi hiyo, alisema serikali iliridhia wananchi wasiondolewe eneo lote la hifadhi bali watengewe eneo la kuishi hekta hizo 3,726.

Vijiji sita ambavyo vimevamia eneo la Hifadhi ya Msitu wa Nindo, vinavyotakiwa kupisha maeneo ya hifadhi na kwenda kuishi katika eneo ambalo wametengewa na serikali ndani ya hifadhi hiyo ni Ng'homango, Mwabundala, Lyamidati, Kadoto, Mwajiji na Buzinza,

# RC aagiza kuwapo dawati la machinga

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, ameziagiza halmashauri zote mkoani Shinyanga kutenga madawati kuratibu kazi zote zinazofanywa na machinga ikiwa ni pamoja na kutatua kero zao.

Mndeme amesema lengo la kufanya hivyo ni kupunguza malalamiko ya wafanyabiashara hao.

Alitoa agizo hilo juzi wakati wa kongamano la Shirikisho la Umoja wa Machinga (SHIUMA) liloandaliwa na wafanyabiashara hao kwa ajili ya kushukuru msaada wa fedha zilizotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan na kueleza kero zao.

Mndeme alisema madawati hayo ya Machinga yatakuwa na kazi ya kuratibu na kushughulikia mafunzo ya ujasiliamali yatakayokuwa yakitolewa ili kuwawezesha katika shughuli zao za kibiashara.

Alisema machinga ni sekta ambayo inasadia katika kukuza uchumi wa Nchi kwa haraka na kuongeza kuwa lazima wawekewe mazingira mazuri ya kukuza biashara zao katika maeneo waliyopo.

Mbunge wa Kahama, Jumanne Kishimba, aliiomba serikali kulitambua kundi la machinga na kulipa heshima kama ilivyo kwa wafanyabiashara wengine wakubwa nchini.

Naye Katibu Mkuu wa SHIUMA, Venatus Anatory, alisema kutokana na kundi hilo la machinga kuwa mstari wa mbele katika uchafuzi wa mazingira, wameamua kuwa mfano katika kuhakikisha mazingira yanatunzwa kwa kupanda miti 10,000 katika maeneo mbalimbali yakiwemo taasisi za serikali na shuleni.

Alisema kuwa tayari wameshasafiri kwenda katika nchi ya jirani ya Rwanda kwa ajili ya kujifunza jinsi ya kutunza mazingira na kuongeza kuwa watakuwa mstari wa mbele kuhakikisha jamii hapa inatunza mazingira.



Ukurasa 12

**BENJAMIN MKAPA 1938-2020**
**Jasiri aliyethubutu kumwonyesha Nyerere upungufu kwenye ujamaa**



Ukurasa 13

BENJAMIN MKAPA 1938-2020
Kuwadi wa utandawazi aliyeinua uchumi Tanzania



Ukurasa 14

**AFRIKA INAPONASWA VITA, MACHAFUKO**
**Miaka 60 ya uhuru inazitegemea bado UN, Ukraine kuilisha 'ugali'**



# Wananchi wanapohisi Tume Haki Jinai ina kazi kubwa kuwarekebisha polisi

**Na Mwandishi Wetu**

KUTOKA Dodoma, Dar es Salaam, Tanga hadi Tabora, kila Mtanzania akiulizwa ana la kusema kuhusu polisi ambao wanaweza kuwa wahusika wakuu kwenye mabadiliko ya taasisi za utoaji haki jinai.

Rais Samia Suluhu Hassan, ameunda Tume ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai, ambayo hivi karibuni imekabidhi ripoti yake na sasa inajipanga kuyafanyia kazi mapendekezo yake kuhusu namna bora ya kuwahudumia na kuwatendea haki wahalifu wa makosa ya jinai.

Ikiongozwa na Mwenyekiti Jaji Mohamed Othman Chande na Makamu Katibu Mkuu Kiongozi mstaafu, Balozi Ombeni Sefue, imeibua mengi lakini ambalo linawagusa jamii ni ukamataji na ushughulikiaji wahalifu ulivyoumiza watu.

Jinai kwa ujumla ni kitendo cha kukiuka au kufanya jambo kinyume na sheria. Huleta madhara, kuondoa amani na haki za raia.

Kwa hiyo sheria, polisi, mahakama, magereza na rumande hutumiwa kushughulika na wanaofanya matendo ya jinai na wale waliopata madhara kutokana na uhalifu ukiwamo wizi, ubakaji, wizi wa kutumia silaha, mauaji, kuharibu mali, rushwa na kughushi.

Katika mjadala wa kuangalia mwenendo wa jinai, polisi wanazungumzwa zaidi, wakidaiwa wanaumiza raia katika mchakato wa kushughulikia uhalifu.

"Inasikitisha kwa sababu watu walitamani kupata msaada kutoka kwa jumuiya au taasisi yenye mamlaka ya kuwatumikia na kuwalinda wananchi pamoja na mali zao lakini ndiyo wamekuwa wakiwafanyia mambo ambayo yamesababisha wadhalilike" anasema mkazi wa Dar es Salaam, anayezungumza na Nipashe.



Rais Samia Suluhu Hassan, akikabidhiwa ripoti ya Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuimarisha Taasisi za Haki Jinai na Jaji Mkuu mstaafu, Othuman CHande. **PICHA: IKULU**

Anaeleza kuwa alikamatwa na kupelekwa kituo cha polisi (jina tunalo) baada ya kupigana sokoni na madalali waliokataa kumlipa baada ya kuwaletea shehena kutoka shambani.

"Nikiwa polisi nikabadilishiwa jalada limeandikwa kesi ya unyang'anyi wa kutumia silaha wala si kupigana. Ndugu waliofika kunidhamini wakakataa jalada la kesi ya unyang'anyi walikuwa waelewa wakapinga na kukataa. Najiuliza hata leo isingekuwa ueelewa na juhudi zao ningekuwa wapi. Nilikuwa nimebadilishiwa kesi na huenda ningefia mahabusu," anadai na kuongeza kuwa ujio wa tume hiyo ni muhimu mno.

Ukingalia ripoti za taarifa za rushwa ('Corruption Watch) za ndani na kimataifa zinawatuhumu polisi kuwa kuna baadhi yao wamekuwa watumishi wa umma wanaoshiriki zaidi ufisadi.

Wanadaiwa kuwa wapo wanaotumia vibaya mamlaka na kupenda zaidi kuogopwa ili kupewa hongo kupitia kubambika mashtaka, kukamata na kutisha ili kuwatoa 'upepo'.

Wananchi wengi wanaunga mkono hatua ya serikali ya kuhakikisha kuwapo na haki kwenye jinai, wakiona ni jambo jema.

Ushauri wao kwa serikali ni wakati mwingine kutoa takwimu za kuonyesha idadi ya watu waliouawa na polisi wakisema ni jambo la kweli kuwa kwa Tanzania siyo rahisi kujulikana.

Na kwa miaka mingi, licha ya kuwa kuna madai kuwa maofisa wa polisi huwaua raia wasio na hatia, lakini mambo hayo ni siri na hayaripotiwi.

Mwaka jana polisi mkoani Mtwara walituhumiwa kuhusika na mauaji ya mfanyabiashara wa madini, wakidaiwa kumchoma sindano ya sumu, lakini wakidai alijinyonga akiwa rumande.

Jeshi la Polisi liliunda kamati ya kuchunguza mauaji, serikali ikapinga, ikaunda tume ya kuchanguza kwa maelezo kuwa polisi haiwezi kujichunguza yenyewe.

Wanatoa mfano kuwa Afrika Kusini mauaji ya raia huwekwa wazi na sasa ni wakati wa Tanzania.

Wapo wanaosema ni jambo baya, kuumiza na kutesa watu na ndicho kinachosababisha wengi kukosa na kupoteza imani na polisi.

Watu sasa wanapaza sauti na kuunga mkono nia ya Rais Samia ya kuweka mfumo mpya kwenye taasisi za haki jinai wakiamini kuwa ni njia pekee ya kuondoa mateso ya wanaohusika na uhalifu.

Wapo wanaoamini kuwa wakati wowote wanapowaona polisi wanakuwa na hofu ya kuadhibiwa, kuteswa na kukamatwa kiholela, hayo ni maelezo ya vijana wanaofanyakazi ya kuosha magari karibu na soko la ndizi Urafiki jijini Dar es Salaam.

"Ni mambo mabaya, vijana wengi wanawakimbia polisi. Inasikitisha kwamba mtu analazimika kuwaepuka wanaopaswa kumlinda, mali na usalama mzima wa jamii. " Anaongeza kijana mmoja.

"Wanaelezea 'tambo' zinazotolewa hadharani kuwa kuingia rumande ni 'bure' lakini kutoka ni lazima 'pesa' tena si kidogo ni nyingi. Watu wanajiuliza mnakamata watu ili kupata fedha?" anahoji.


Ukiangalia nguvu zinazotumiwa na polisi zinaonekana zaidi kwenye maeneo au makazi ya watu wenye maisha duni au maskini , wakazi wa Buguruni SPENCO wanaiambia Nipashe, wanapozungumzia suala la marekebisho ya mifumo ya taasisi za jinai.

Wanasema huko kuna bangi, dawa za kulevya, kupora, kufanya, mauaji, vipigo na kusababisha maeneo kuwa 'viwanda vya uhalifu' kunakolazimisha polisi kutumia nguvu ya ziada na kuwakabili.

Wanapendekeza tume ya Rais ifike maeneo ya wenye kipato kidogo na makazi duni kushauriana nao ili kufahamu namna bora ya kuwalinda na kuwasaidia wanaotenda jinai kwenye sehemu hizo ambao mara nyingi wameathirika na misako ya polisi dhidi ya wahalifu.

# Jasiri aliyethubutu kumwonyesha Nyerere upungufu kwenye ujamaa

**Na Ani Jozeni**



RAIS mstaafu Benjamin Mkapa aliondoka duniani Julai 24 mwaka 2020, akiwa na miaka 81. Ni mmoja wa wasaidizi wa 'awamu ya pili' ambayo ilikuwa ya waasisi wa TANU na muunda serikali Mwalimu Julius Nyerere, kwa maana ya kuingia katika uhusiano wa kikazi miaka ya awali baada ya uhuru.

Itakumbukwa marafiki na washirika wa Mwalimu wa awamu ya kwanza ni wale aliokutana nao wakati TANU inaanzishwa hadi uhuru kupatikana, ikiwa ni pamoja na Rashidi Kawawa, Amir Jamal, Pius Msekwa, George Kahama, Paul Bomani na Timothy Apio.

Maswahiba wengine wa kundi la pili ni pamoja na John Malecela, Cleopa Msuya na Benjamin Mkapa ila tofauti ni kuwa Mkapa awali alikuwa mmoja wa wanafunzi bora wa Nyerere wakati akifundisha Pugu Sekondari.

Licha ya makundi haya siyo tofauti sana kiumri, kisiasa yalikuwa na tofauti ya wazi kwani waliokuwapo miaka ya 1950 waliingia madarakani wakiwa vijana zaidi na wale wa baadaye ilibidi wangoje kiasi, kupata nafasi zilizo wazi. Hivyo walianzia katika ngazi za utawala ingawa kimsingi zilikuwa ni za juu, wakaingia serikalini miaka ya 1970.

Mwaka 1977 Mkapa aliingia serikalini akiwa amepitia nafasi tofauti kama msaidizi wa karibu wa Mwalimu hasa katika masuala ya habari, akianzia uhariri Redio Tanzania, gazeti la The Nationalist, Standard ambayo leo ni Daily News. Shirika la Habari -SHIHATA na mwishowe Mwandishi na Msemaji Ikulu.

Alipoingia madarakani mwaka 1995, baadhi ya wachambuzi hasa nchi za nje wakaanza kusema 'mwanahabari aukwaa urais Tanzania,' wakasahihishwa na mwanahabari mkongwe Jenerali Ulimwengu, aliyefanya kazi kwa muda mfupi na Mkapa akiwa bado magazetini.

Anafafanua katika makala 'The East African' kuwa Mkapa hakuwa mwanahabari wa kawaida, 'he was always the boss,' yaani alianzia uanahabari juu kileleni na kubakia huko au kupanda juu zaidi. Hivyo pamoja na kuwa hulka ni hisia za mtu binafsi ni kweli kuwa makada waliotoka vyuo vikuu wakati huo hawakupata muda wa kunyenyekea, walianza moja kwa moja pale juu, kubaki hapo maisha yao yote serikalini.

Moja ya maeneo yaliyomsaidia Mkapa kukua na kufikia ngazi za juu ni umahiri wake wa kuzungumza Kiingereza, uliomwezesha kumwelewa Nyerere kwa kina wakati washirika au aliokuwa anafanyao nao walikuwa wagumu, alilazimika kuanzia katika uwanja mpana zaidi, kwa mfano itikadi ya mapinduzi katika Azimio la Arusha au Mwongozo wa TANU.

Mkapa hakuhitaji kuelezewa kwa kina nini tofauti ya 'uhuru' ambayo ni fikra ya msingi ya Mwalimu, na mapinduzi. Wateule wa Mwalimu katika nafasi ya uwaziri wa mambo ya nje, alipoondoka Oscar Kambona, walikuwa wanakwama hapo, wakijichanganya hasa kwenye hadhara za kimataifa.

Walibakia mawaziri wa nchi kutoka 1967 hadi 1977 alipoingia Mkapa akiwa kama waziri kamili wa Mambo ya Nje.

Kuna kibwagizo kingine kinachoweza kutoa picha ya urais wa Mkapa ulipotokea, kuwa hata wale waliotangulia serikalini awamu ya kwanza, walishakiri wakati fulani kuwa ndiyo kiongozi wao ila hawakujua kuwa ndicho wanachokifanya.

Hadithi iliyowahi kuelezwa na waliokuwa karibu na watawala nyakati za awamu ya pili zilisema kuwa mwaka 1980, baada ya vita na Iddi Amin wa Uganda halafu kukawa na hali ngumu ya uchumi, kundi la mawaziri likamtaka Mkapa kumweleza Mwalimu umuhimu wa mabadiliko kwani Ujamaa na Kujitegemea ulionekana unaikwamisha nchi.

Mwalimu inasemekana alimshangaa Mkapa kwa kuwasilisha maoni yale, akamuunganisha nayo, akamtoa uwaziri akampeleka ubalozini ng'ambo. Ina maana kuwa mwaka 1995 wakati wa kutafuta mrithi wa Ali Hassan Mwinyi, aliyechukua nchi baada ya Nyerere suala hilo lilikuwa limeshafungwa, kwani mawaziri wa nyakati zile ambao wengi waliingia miaka si chini ya 15 kabla ya hapo walikuwapo katika kundi lililomtuma Mkapa awawakilishe kwa Mwalimu.

Mkapa akakinywea kikombe hicho, akaubeba msalaba wake akaondolewa serikalini, ila akawa amethibitisha ujasiri na uwezo wa kusikiliza wengine, na kutumika hata katika kupeleka ujumbe hatarishi kwa mkuu wa nchi.

Hivyo yale maneno eti Mkapa aliinuliwa tu na Nyerere, ni kijana wake hayatoshi, ni lazima kukumbushia wenzake walivyomtwika uongozi, 1980.

Eneo jingine ambalo unaweza kusema linaendana na hilo ni jinsi ambavyo ukaribu wake na Mwalimu na usomi au udiriki wake binafsi ulivyomweka rais huyo mstaafu katika nafasi ya urais.

Waliomfahamu kwa uthubutu wake katika diplomasia na hata kisa hicho cha 1980 walitazamia kuwa amejengeka kiasi cha kufanya maamuzi yake mwenyewe, kile kinachoitwa 'maamuzi magumu.'

Ila waliomfahamu kwa historia pana zaidi ya kuwa mwanafunzi wa Nyerere na msaidizi wake wa karibu muda wote akiwa madarakani waliamini atakuwa mtu sahihi kusimamia maadili, misingi, mafundisho ya Mwalimu kwa jumla.

Ndiyo hapo unapata mihimili ya uthubutu na vile vile udhaifu wa awamu ya tatu, kuendesha farasi wawili kwa wakati mmoja, kusimamia itikadi ya CCM kwa maeneo mengi, makada na wengi kati ya wasomi wakitaka ajitenge na hulka ya 'soko holela' ya awamu ya pili.

Hilo alilifanya kwa ufanisi kwa kuunda mifumo ya usimamizi wa uchumi na kuteka itikadi ya wafuasi wa Mwalimu alipolikaba koo 'soko holela.'

Isitoshe akawakirimu watawala serikalini kwa kuwaruhusu kupanga walichotaka, kwa mfano kulinganisha mishahara ya wataalamu wa ndani mashirika ya umma na wanaotoka nje, hivyo mkurugenzi mkuu au mtendaji wa mashirika kama TANROADS, Shirika la Maendeleo ya Petroli TPDC, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari kwingine akawa anatazamia Shilingi milioni 12 na baadaye kupanda hadi milioni 40.

Rais wa awamu ya tano ni 'mwanae' wa kisiasa, ndiye John Magufuli, aliyeufumua kwa kiasi si kidogo mtindo huo, licha kutokuwapo na uwazi, na si rahisi kusema ni kwa kiwango hali ya awali imerudi. Japo unaweza kusema kuwa mfumo aliouweka Mkapa ndiyo ulikuwa unawafaa zaidi watawala serikalini ila ukajenga hisia za chuki, watu wakiona wakubwa wanaofaidi kupita kiasi, wanaanza kutimkia upinzani kuleta mabadiliko.

Alijitahidi vilevile kuendana na hisia za chama tawala ambacho hakijawahi kufikiria kuachia ngazi za utawala kupitia sanduku la kura, licha ya kuwa uwezekano huo ulikuwa wazi zaidi kwa upande wa Zanzibar, na hali hiyo inaelekea ilifikiwa 1995 halafu 2015.

Nyakati zote mbili kulikuwa na taarifa tata za vyombo vya habari kuhusu ujumlishaji kura na matokeo ya awali, baadhi ya wahariri wakahojiwa kwa kuchapisha au kutangaza kwenye runinga taarifa za uchaguzi za kuokoteza.

Alibaki na hisia za kusononeka kwa mfano baada ya mauaji ya waandamanaji upinzani Zanzibar Januari 2001, ila alibanwa na mfumo, akawa mkali akiulizwa maswali. Alikiri kuteswa na tukio hilo katika kitabu cha kumbukumbu yao maisha yake ila msingi wake asingeweza kuujutia.

Akitangaza kifo cha Mwalimu Oktoba 14, 1999, pamoja na mambo mengine, Rais Mkapa alisema 'baada ya kuondoka Mwalimu, wale tulioachiwa hatamu za uongozi wa nchi, tutaulinda Muungano kwa nguvu zote." Hapakuwa na nafasi ya kufanya kinyume.

BENJAMIN MKAPA 1938-2020

# Kuwadi wa utandawazi aliyeinua uchumi Tanzania

**Na Gaudensia Mngumi**

JUMATATU ya juma hili, ilitimu miaka mitatu tangu kutangazwa kifo cha Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa.

Baada ya mihula miwili mfululizo inapotimia miaka 10, alistaafu kufuatia uchaguzi wa Desemba 2005, akijulikana kama mwanasiasa mahiri na kwa kiasi kikubwa 'pengine msoshalisti'.

Kiongozi huyo aliyeongoza kuanzia 1995 hadi 2005, alifariki dunia Julai 24, 2020 , hivyo ni miaka mitatu tangu kutwaliwa kwenye dunia hii.

Hata sasa, anakumbukwa kwa mengi. Alipochaguliwa alitarajiwa kuwa angeendeleza usoshalisti kwa vile alikuwa mwanafunzi wa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, lakini hakutukuza ujamaa, badala yake akaukumbatia uliberali na soko huri, na baada ya muongo wa uongozi wake, akaiacha Tanzania ikiwa imeimarika kiasi kiuchumi.

Wapinzani wa Mkapa hapo awali walimpachika jina la kijana wa Nyerere na kumtazama kuwa asingeweza kuiondoa minyororo ya ujamaa na kuibadilisha nchi, iliyokuwa imedorora zaidi kiuchumi wakati anaingia ikulu 1995.

Ingawa hakuitupa itikadi ya ujamaa, Mkapa alikumbatia sera za kibepari kwa nguvu zote. Hii ilimletea sifa kutoka kwa taasisi za mikopo za kimataifa kama Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), lakini nyumbani akapondwa na akaonekana kama kuwadi wa utandawazi na dalali wa mali za umma hasa mashirika aliyoyauza kwa wawekezaji wageni.

**KUJENGA UCHUMI**

Mihula miwili ya Mkapa madarakani iliibadilisha Tanzania kiuchumi, ingawa mengi zaidi hata sasa yanahitajika kufanyika ili nchi iwe na misingi ya kiuchumi imara.

Mwanzoni anapoingia uongozini, aliazimia kwa dhati kufufua uchumi, kuleta mageuzi ya kimuundo, ikiwa ni pamoja na sera ya ubinafsishaji iliyoanzishwa na mtangulizi wake, Ali Hassan Mwinyi.

Mkapa alishangaza kwenye kasi ya kuleta mabadiliko, mwaka 2004 mfumuko wa bei ulifikia karibu asilimia nne (4) mwenyewe akiita 'single digit inflation' ikilinganishwa na asilimia 27.1 ya mwaka 1995.

Ukuaji wa uchumi kwa mwaka ulifikia asilimia 6.7 mwaka 2004, kutoka asilimia 3.6 wakati Mkapa akichukua uongozi 1995 na ilipofikia mwaka 2005, akiba ya fedha za kigeni iliongezeka hadi kufikia miezi minane ya uagizaji bidhaa kutoka nje na makusanyo ya mapato yalifikia dola za Marekani milioni 140 kwa mwezi, zaidi ya mara tatu ya kiasi cha mwaka 1995-1996.

Ni taarifa alizozitoa wakati akihutubia bunge , Julai 14 ,2005, wakati huo anatoa majumuisho ya mihula miwili ya uongozi wake ili kuachia ngazi na taifa lijipange kwa uchaguzi mkuu wa 2005.

Mkapa anawaaga wabunge kwa kuwaambia kuwa utawala wake umeimarisha uchumi mkubwa (macro economy) jambo linaloongeza imani ya wawekezaji kwa nchi na kwa serikali, tofauti na hali ilivyokuwa wakati alipochaguliwa kuwa rais.

Alikuwa akitamba kuwa sera za Tanzania aliyokuwa anaiongoza zilifanikisha kupata msamaha na kufutiwa madeni hivyo

Benki ya Dunia na IMF, Novemba 2001 zikafuta zaidi ya deni la dola bilioni 2 ikiwa ni takriban nusu ya kiasi ambacho nchi ilikuwa inadaiwa.

**ALIKUBALI WAKOSOAJI**

Alikosolewa kuwa asijidai kuwa Tanzania imefuzu kuwa nchi maskini na yenye mzigo madeni makubwa na kwamba umaskini si sifa kwa taifa lenye rasilimali kama hilo analoliongoza.

Wakosoaji wake walimponda, akionywa asijisifie kuwa amefutiwa madeni kupitia mpango wa Heavily Indebted Poor Countries (HIPC) kwa kuwa umaskini si ufahari wala kitu cha kujipatia heshima.

Mkapa ni maarufu kwenye ubinafsishaji taasisi kadhaa za serikali kama vile Benki ya Biashara NBC , iliyodaiwa kutolewa 'bure' kwa benki ya Afrika ya Kusini ya ABSA Group Limited, hapo ndipo wakosoaji wake walimponda kuwa anachokiita mafanikio ya kiuchumi ya nchi hiyo si kitu zaidi ya giza nene.

Walisimamia ukweli kuwa ubinafsishaji haukuwainua Watanzania ikielezwa kuwa sehemu kubwa wakati huo watu milioni 36 walikuwa wakiishi chini ya dola moja kwa siku.

"Kuendelea kwa umaskini nchini , hasa katika maeneo ya vijijini, kunatia wasiwasi," anakosoa mgombea urais Ibrahim Lipumba, mchumi na Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi CUF, ambaye alikuwa mpinzani wa Mkapa kwenye uchaguzi mkuu wa na 1995 na 2000 lakini akishindwa.

Mwanasiasa mwingine Freeman Mbowe wa CHADEMA, alimpa Mkapa za uso, akimwambia kutokana na umaskini Watanzania hawana cha kujivunia baada ya miaka 44 ya uhuru.

"Angalia, kuna vijiji vingi ambavyo haviwezi kufikika kwa mwaka mzima kutokana na ukosefu wa barabara bora, wengi hawana huduma bora za afya, na wakulima wanashindwa kufika sokoni na mazao yao," anasema Mbowe.

"Tukiwa na umaskini kote, tunashuhudia wanasiasa na viongozi wakuu wa serikali wakituna ndani ya magari ya bei mbaya. Anasema Mbowe akipinga serikali ya Mkapa kukumbatia magari ya kifahari au 'mashangingi' tena yakiitwa V8, ikielezwa kuwa ni gharama kubwa kwa nchi hii maskini .

Mkapa alikubaliwa kukosolewa, lakini akasisitiza kuwa anaondoka madarakani akiwa na furaha, baada ya kujenga barabara maeneo mengi ya nchi na ikiwa sera zake zitadumishwa baada ya kuondoka kwake, kuna uwezekano mkubwa kwamba mikoa na wilaya nchini zitaunganishwa na barabara za kisasa miaka inayokuja.

**TEHAMA**

Mkapa pia ameichia Tanzania sekta imara ya mawasiliano na simu za mkononi kwa wingi na kwamba eneo hilo limekuwa kwa kasi na nchi kuwa na sifa kwenye matumizi ya simu na mitandao ya internet.

Tanzania sasa ni mojawapo ya soko la simu za mkononi linalokuwa kwa kasi barani Afrika, takribani wateja milioni 46. Wanatumia simu za mkononi kwa kwa mujibu wa ripoti ya karibuni ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano (TCRA).

Mkapa alipoondoka ikulu aliiachia nchi benki 30 zikiwa za biashara, za kijamii, maduka mengi ya kubadilisha fedha na taasisi kadhaa za kifedha zisizo za benki za kutoa mikopo midogo na mikubwa licha ya kwamba imebandikwa majina ya mikopo umiza kausha damu na majina kama hayo.

Juhudi zinaendelea ili kuimarisha utoaji wa huduma za kifedha kwa watu wengi vijijini kwa kuwa mtandao wa kibenki bado upo kwenye majiji hasa Dar es Salaam na miji mingine mikubwa.

Benki hizo pia zinahudumia wateja wa mijini, wafanyabiashara na wasomi zikiwaweka pembeni mamilioni ya wakulima, wachimbaji madini na wavuvi katika maeneo ya vijijini na kuilazimisha serikali kuwa na mikopo ya wajasiriamali ikinufaisha vijana, walemavu na wanawake.

**BABA WA ELIMU**

Katika moja ya makongamano wakati wa siku za mwanzo za utawala wake, Mkapa alisema, kuna mapungufu katika elimu na kuja na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi MMEM, ambao uliwaingiza watoto wengi wenye umri wa kwenda shule madarasani.

Akiboresha pia sekondari kupita mpango wa MMES na kuwafikia wanafunzi waliokosa fursa ya kusoma kupitia programu ya MEMKWA.

Licha ya kuwapo uhaba wa vyumba vya madarasa, madawati, maabara, mabweni na walimu, elimu ya msingi ilipatikana karibu kote nchini, kadhalika sekondari nazo ziliongezwa na mafanikio yakaanza kuonekana.

Awamu yake iliruhusu watu binafsi, mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi za kidini kuanzisha shule katika ngazi ya msingi, sekondari na elimu ya juu. Shule hizo zinazidi kushamiri, na mwelekeo unaonyesha kuwa Watanzania wanaweza kuwa na hata vyuo vikuu viwili katika kila mkoa kwa vile sekta binafsi ilipewa nafasi.



## AFRIKA INAPONASWA VITA, MACHAFUKO

# Miaka 60 ya uhuru inazitegemea bado UN, Ukraine kuilisha 'ugali'

**Na Nimi Mweta**

UMOJA wa Afrika (AU) unailalamikia Urusi kwa kufunga njia ya bahari ya kuuza ngano na nafaka nyingine yakiwamo mafuta ya kupikia ya bei nafuu bidhaa zote zikitokea Ukraine.

Ndizo zinazoelezwa kuwa ni bidhaa tegemeo kwa serikali kadhaa katika ukanda wa Kaskazini wa Afrika, na mashirika ya Umoja wa Mataifa (UN) yanayohitaji ngano kwa maeneo ya vita na kusaidia makambi ya wakimbizi barani humu.

Mzigo ulikwishakuwa mkubwa hata kabla ya hatua ya Russia kufunga njia hiyo hivyo taabu inaelezwa kuwa ikazidi zaidi.

Jambo ambalo siyo rahisi kulielewa ni kwanini Afrika, yenye ardhi yenye rutuba ya kulima kuliko bara lolote duniani iwe tegemezi tena kwa kiwango kikubwa, kwa nafaka kutoka nje tena Ulaya?

Ka mfano Ethiopia ni taifa lenye ardhi yenye rutuba zaidi duniani ikiwa ndiyo nyumbani kwa mito miwili Nile na Blue Nile, lakini kuna Ghana, Sudan Kusini, Morocco na Congo DRC, ambazo zinatajwa na ripoti ya mtandao wa African markets ya mwaka huu.

Kabla ya vita wengi barani humu walikuwa hawana habari za ni kwa kiwango gani bara lao linategemea nafaka kutoka nchi hiyo ya Ulaya Mashariki, iliyokuwa na wakazi milioni 43.7 hadi mwaka 2021. Licha ya kuwa ndani yao dimbwi la vita vikali ya jirani yake Urusi bado ni tegemeo la mashirika ya kimataifa na masoko kwa nafaka.

Hoja nyingine ya kujiuliza ni kitu gani kinachozuia nafaka isizalishwe Afrika? Hata kama inapatikana nchi yenye ardhi tele na amani, mvua za kutosha na mabonde na mito mingi kama Tanzania?

Na kwa upande mwingine kwanini takriban kila nchi barani humu inakwama kisiasa na kuingia katika machafuko, kupigana itegemee chakula siyo tu kutoka nje, ila kiletwe kama msaada na mashirika ya UN? Unaweza pia kuongeza swali kama uwezo wa Afrika kufikiri umeishia hapo au inaweza kujinasua?

Njia rahisi ya kutatua suala hilo ni kuweka vigezo vya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, mwaka 1967 katika Azimio la Arusha, na kuangalia ni kwa kiwango gani au kwa njia gani viwango hivyo vinawezesha kuelewa hali hiyo, na jinsi ya kuitatua.

Mwalimu alisema 'ili tuendelee tunahitaji vitu vinne - watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora.' Wasomi wa Afrika kwa urahisi tu wanakubaliana kuhusu hitaji la uongozi bora, na hakuna uhakika kama 'siasa safi' inayoweza kuiwezesha kuwako na tija ya kilimo kama ilivyo Ukraine. Si rahisi kuona Afrika ianze kujiuliza swali kama hilo.

Labda kwanza tupate jibu la swali hilo kabla ya kuanza kuangalia ni wapi Afrika inakwamna, hata kujiuliza swali hilo, kuanza na uelewa wa Mwalimu katika maelezo hayo, unakuta kuwa ni mfumo kama huu uliopo anaotazamia utaleta maendeleo, yaani watu kumiliki ardhi wao wenyewe, na serikali kusimamisha uzalishaji kwa hatua tofauti, kwa mfano vyama vya ushirika, mikopo ya pembejeo au vifaa vya kilimo.

Hitaji la uongozi bora kimsingi linaendana na hilo la siasa safi, kwani kama hakuna uwezekano wa tija katika uchumi, siasa itagubikwa na mitafaruku.

Ndiyo hali ambayo imetawala tangu uhuru, kuwa hakuna uwiano kati ya tija ya uzalishaji Afrika na mahitaji ya kuendesha nchi. Licha ya kuwa aina tofauti za udhaifu kama ubadhirifu katika manunuzi idara za serikali au mashirika ya umma, usingeweza kuwa chanzo cha mkwamo wa kiuchumi, na lingekuwa jambo rahisi kutatua masuala kama hayo kisiasa, si kuanza vita kwa sababu hiyo.

Mifarakano inatokana na ulazima wa kuchukua hatamu za dola kwa maslahi ya tabaka hili au lile, au mfungamano wa kitabaka, na sababu ya msingi ni kukosekana tija katika uchumi na mahitaji ya umma.

Kukimbilia haraka katika jawabu na halafu kuangalia kama Afrika inaweza kufika hapo, tujikumbushe kibwagizo katika mdahalo wa dunia kuhusu maendeleo, cha mwaka 1981.

Alipoingia madarakani rais mhafidhina wa Marekani, Ronald Reagan, akaanzisha mpango wa mabadiliko makubwa katika sera za Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), nchi zinazoendelea ziliitisha mkutano nchini Mexico na sita kati ya nchi hizo zikatoa wakuu wake wa serikali au nchi, kukutana ana kwa ana na Rais Reagan kuhusu mustakabali wa maendeleo duniani.

Kimsingi jambo hilo ni muhimu zaidi sana kuliko hata wakati huo, licha ya kuwa kwa Tanzania tumepiga hatua ukilinganisha na 1981, na nchi nyingi za Afrika, kama si zote, zitasema hivyo pia.

Mwalimu alipata nafasi ya kuongea na Reagan na inasemekana rais huyo wa Marekani akamwambia kuwa anaweza kupeleka wakulima wanne kutoka Marekani, Nyerere awape ardhi ya kutosha walime kwa 'combine harvesters' na kuilisha Tanzania. Mradi tu wamilikishiwe ardhi, watafute mikopo benki.

Hakuna ubishi kuwa Mwalimu asingekubali pendekezo hilo na hata hivyo Reagan hakuwa anataka kuleta wakulima hao, ila ni kukumbushia kuwa umaskini wa Afrika ni kukosa kujituma, kukataa mifumo yenye tija.

Ila kabla ya kufika hapo, tuangalie wazo hilo katika hali tofauti, pale 'mwanae Mwalimu' wa kisiasa, Rais Benjamin Mkapa, alipomkaribisha Profesa Hernando de Soto wa Peru kuzungumzia tija katika uchumi kwa uandikishaji na umilikishwaji wa ardhi.

Watawala wakafurahia dhana hiyo ila wakaipindisha iendane na vigezo muhimu vya uzalendo wa Afrika ndicho kinachoitesa Tanzania ambako kwa takwimu za hivi karibuni mikoa takriban 19 inahitaii misaada ya chakula (siyo tu kupelekewa wanunue) wakati kuna ardhi tele, mito na maziwa, na hakuna machafuko.

Afrika mzima kimsingi inataka ilishwe kwa mpira na nchi za Magharibi, na inachoweza ni kuanzisha mafarakano kubadili utawala ili wengine wafaidi, na siyo kuweka misingi ya umiliki ardhi yenye tija, ivute mikopo ya benki, wajasiriamali waenee kila mahali wazalishe kwa mitambo ya kisasa, nafaka iuzwe bei rahisi.

Ikifikia hapo, chakula kinapokuwa rahisi na bidhaa nyingine zinakuwa rahisi kwani mshahara hautumiki tena kwa sehemu kubwa kununua chakula. Ila ni umiliki binafsi nchini kote, siyo kukodishia wawekezaji; haitapita mwaka kabla ya wenyeji kuidai ardhi hiyo ya jadi.

Kwa maana hiyo kinachoimaliza Afrika ni mifumo ya jadi ya umiliki ardhi ambako wamiliki wanapata taabu hata kuzalisha chakula chao wenyewe na kupata fedha za kutosha kwa mahitaji ya ziada, labda waongeze biashara. Hatua kwa hatua hali hiyo inabadilika lakini haiwezi kuleta tija kubwa ndani ya muda mfupi kwani ni kilimo cha mbinu endelevu mbegu bora, umwagiliaji, pembejeo na utaalamu ila cha watu wachache, kutosheleza hitaji la nafaka nchini.

Matokeo yake maelfu ya vijana wanajaribu kutimkia ng'ambo maisha yanapokuwa magumu, na wanajua Wazungu hawana familia kubwa. Hivyo wanahitaji watu wa kufanya kazi hata za hali ya chini, kwani fedha itatosha.

Afrika inahitaji kujua kuwa mali binafsi katika ardhi, uraia wa nchi mbili na soko huria la kila kitu, ili ardhi inunuliwe na wale walioko nje wenye fedha, walime kwa mitambo mikubwa, halafu sekta kuu za uchumi ziingie mikono ya watu binafsi ziinue tija kama ilivyo kwa simu za mkononi.

Wasomi Afrika wakisikia mfumo huo wanatoa laana, wasijue kuwa nchini Marekani ni asilimia tano ua raia wake inayotegemea kilimo,na wanatoa zaidi ya robo ya nafaka yote inayozalishwa duniani. Tija katika matumizi ya ardhi na kuondoa mashirika ya umma yanayozitesa nchi za Afrika kwa madeni ya nje ni njia rahisi ambayo inaikataa, hivyo inakula jeuri yake.



Moussa Faki Mahamat, Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika. **PICHA: MTANDAO**



## Mbunge ataka makandarasi wazembe kuchukuliwa hatua

**Na Paul Mabeja,** KONDOA

MBUNGE wa Kondoa Vijijini, Dk. Ashatu Kijaji, amekiomba Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwachukulia hatua makandarasi ambao wameshindwa kukamilisha miradi ya maji licha ya kulipwa stahiki zao zote.

Alitoa ombi hilo juzi wilayani hapa kwa Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Tanzania Bara, Abdulrahiman Kinana wakati wa kikao cha kutathimini utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema hivi sasa kero wanayokabiliana nayo ni wakandarasi ambao wamekuwa wakikwamisha miradi ya maji licha ya serikali kuweka fedha nyingi kwenye miradi hiyo.

"Changamoto ni wakandarasi katika sekta ya maji. Hapa Kondoa tunayo Sh. bilioni 15 lakini kiasi hicho huwezi kuona uhalisia wake kwenye maisha ya wakazi wa wilaya hii kwani miradi mingi inakamilika lakini haitoi huduma na fedha zinakuwa zimekwisha, hivyo tunakuomba chama kiingilie kati ili tupate wakandarasi wenye uwezo na sisi wananchi wetu wafaidi matunda ya serikali yao"alisema

Dk. Ashatu ambaye pia ni Waziri wa Viwanda na Biashara alisema wanaiomba serikali kuwapatia msaada wa chakula cha bei ya ruzuku ili kusaidia wananchi ambao wengi wao wanakabiliwa na uhaba wa chakula kutokana na kukosekana kwa mavuno ya kutosha katika msimu huu wa kilimo.

"Tunaishukuru sana serikali ilituletea chakula cha bei ya ruzuku lakini hali inaonyesha kuwa mwaka huu hali itakuwa mbaya zaidi, hivyo tunaiomba serikali kutuletea chakula cha msaada kwa bei ya ruzuku ili kusaidia wananchi wetu wanaokabiliwa na uhaba wa chakula"alisema Dk. Kijaji

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya CCM wa wilaya hiyo katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan alisema wameshapokea Sh. bilioni 32.3 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Dk. Ashatu alisema hakuna kijiji ambacho hakijaguswa hadi sasa katika miradi ya maendeleo ikiwemo ya elimu, afya, maji, pamoja na miundombinu ya barabara. "Katika sekta ya elimu hivi sasa hakuna watoto wanaotembea umbali mrefu kwenda shule katika kipindi hiki cha uongozi wa Rais Samia. Tumeshapokea Sh. bilioni saba, haijawahi kutokea tangu nchi yetu kupata uhuru"alisema Dk. Kijaji

Naye Mbunge wa Kondoa Mjini, Ally Makowa, alisema wanaiomba CCM kuingilia kati tatizo la wakandarasi kushindwa kukamilisha miradi ya maji ambayo serikali imetoa fedha.

# CCM yawaita wadau kutoa maoni mkataba wa Bandari

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amesema serikali ya chama hicho inakaribisha maoni na michango yenye tija kutoka kwa watu mbalimbali ili kuboresha mkataba wa uwekezaji wa Bandari ya Dar es Salaam.

Aliyasema hayo juzi wakati wa mkutano wa hadhara wa kutoa elimu ya makubaliano ya Serikali ya Tanzania na Dubai kuhusu uendeshaji wa bandari ya Dar es Salaam uliowashirikisha wananchi kutoka mikoa ya Singida, Dodoma na Tabora.

"Tuko imara, tunaruhusu maoni na michango yenye tija ili kuboresha mkataba wa bandari ya Dar es Salaam sababu lengo letu ni kutafuta matokeo chanya sio majungu na uzushi usiokuwa na maana," alisema.

Chongolo alisema wanaopinga uwekezaji katika bandari ya Dar es Salaam hawana hoja ya msingi na kwamba kwenye dunia ya sasa wananchi wanapaswa kutambua kuwa Tanzania ipo kwenye vita ya ushindani wa kiuchumi na mapambano ya maendeleo ambapo kila taifa halitaki kuona Tanzania inakuwa kimaendeleo.

"Vita ya uchumi ni vita inayotutaka tukae mguu sawa kwa sababu maeneo au fursa wanazohangaikia ndio hayo hayo ambayo na sisi tunahangaikia, hivyo tusikubali kuyumbishwa kwa maeneo ya uwongo," alisema.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Prof.Kitila Mkumbo, alisema uwekezaji wa bandari ya Dar es Salaam utakuwa na manufaa makubwa kwani mapato yatokanayo yataongezeka kutoka Sh.trilioni 7.7 hadi Sh. trilioni 26.7.

Alisema bajeti ya serikali iliyopitishwa na Bunge mwaka huu ni Sh.trilioni 44, kati ya hizo Sh.trilioni 26 zinakusanywa na serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na zinazobaki serikali inalazimika kukopa au kuongeza tozo.

"Wataalamu wamebaini tukifanya uwekezaji mzuri wa Bandari ya Dar es Salaam mapato yataongezeka kutoka Sh.trilioni 7.7 na kufikia Sh.trilioni 26.7 hivyo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) itakuwa na uwezo wa kukusanya Sh. trilioni 52 zaidi ya bajeti ya serikali na hivyo kuondoa mzigo wa kutozwa kodi kwa Watanzania, "alisema.

Pro.Mkumbo alisema uwezo wa Bandari ya Dar es Salaam ni kuhudumia mizigo tani milioni 21 kwa mwaka lakini uwekezaji utakapofanyika itakuwa na uwezo wa kuhudumia mizigo tani milioni 50 kwa mwaka.

Kuhusu madai ya mwekezaji kupewa bandari yote, alisema siyo kweli Kwa sababu bandari ya Dar es Salaam ina maeneo matatu, eneo la kwanza ni la ndani ambalo lina ukubwa wa hekta 106, eneo la Kurasini hekta 51 na eneo la tatu ambalo lipo Kibaha lina hekta 500.

"Mwekezaji ndani ya bandari ya Dar es Salaam atapewa hekta 7.7 atapewa magati kuanzia sifuri hadi nane na magati mengine watapewa wawekezaji wengine ili washindane, na tija itaongezeka na mwekezaji akishindwa kuleta ufanisi ataondolewa na hilo lipo wazi ndani ya mkataba," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Singida Peter Serukamba, alisema wanaopinga uwekezaji wa bandari ya Dar es Salaam ni kutokana na kasi ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuleta maendeleo, hivyo wanahofu watakosa cha kusema hasa katika kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Serukamba alisema amefanikiwa kuusoma mkataba huo, kwamba kipo ibara ya 14 hakisemwi na wanaopinga mkataba huo ambacho kinaeleza kuwa iwapo mwekezaji atashindwa kutekeleza vizuri, serikali imepewa mamlaka ya kuvunja mkataba na mwekezaji hawezi kwenda kushtaki sehemu yoyote.

"Rais Samia Suluhu Hassan ni mwanauchumi anajua nini kifanyike katika kuinua uchumi wa nchi, hivyo suala la uwekezaji Bandari ya Dar es Salaam kinachofanyika ni kutaka kuinua uchumi wa nchi hivyo wanaopinga uwekezaji huo hawaoni mbali," alisema.

Serukamba alisema duniani mambo yamebadilika ili watu waje wawekeze sehemu ni lazima mwekezaji aje afanye utafiti.

Hivyo aliwaomba wananchi kuendelea kuunga uwekezaji wa Bandari ya Dar es Salaam na kupuuza wanaopinga.



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba (kushoto), akitoa maelekezo kwa Ofisa Ardhi wa Wilaya ya Manyoni, Emmanuel Mdemwa (kulia), wakati wa mkutano wa kusikiliza kero za wananchi wa kitongoji cha Majengo, kata ya Manyoni juzi, waliolalamikia kukithiri kwa migogoro ya ardhi katika wilaya hiyo. Katikati ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Jimson Mhagama. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# TFRA yamulika ubora wa mbolea

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BODI ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) imewaagiza wamiliki wa viwanda vya mbolea nchini kuzalisha bidhaa bora zenye viwango ili kuepusha malalamiko kutoka kwa watumiaji. Agizo hilo limetolewa juzi na Mkurugenzi wa bodi hiyo, Thobias Mwesiga katika kikao baina ya wajumbe wa bodi hiyo pamoja na menejimenti ya TFRA kilichofanyika mwishoni mwa wiki kikiwa na lengo la kuhamasisha uzalishaji wa bidhaa hiyo katika mikoa tofauti.

Alisema ili kuepuka hayo wawekezaji wanapaswa kuzoea kukaguliwa na mamlaka hiyo ili kuhakikisha viwango vilivyokubalika ndivyo vinaingizwa sokoni.

Mwesiga alisema jukumu la ukaguzi wa mara kwa mara kwa wawekezaji wa viwanda utakuwa endelevu, lengo ni kuwakumbusha kuzingatia vigezo vya uzalishaji ikiwemo ubora wa bidhaa hiyo kwa watumiaji.

"Suala la ukaguzi wa mbolea linalofanywa na TFRA lizoeeni maana litafanyika sana tunahitaji kuona bidhaa bora za mbolea zinazalishwa,"alisema Mwesiga. Akizungumzia kuhusu uzalishaji aliwataka wazalishaji wa ndani wa mbolea kuzingatia ubora wa bidhaa zao kabla hawajazipeleka sokoni ili kulinda afya za watumiaji.

Alisema ili mbolea ipate kibali cha kuuzwa ndani na nje ya nchi ni lazima iwe na vyeti vinavyothibitisha ubora wa bidhaa kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS), lakini pia vibali vyote kutoka mamlaka zinazosimamia tasnia hiyo. Aidha, alisema pia inapaswa iwe imekidhi matakwa ya Sheria ya Mbolea inayosimamiwa na TFRA pamoja na matakwa ya mamlaka nyingine kama vile, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali na nyinginezo.

Hadija Jabir, mjumbe wa bodi hiyo, aliwataka wawekezaji kuona namna wanavyoweza kuwasaidia wakulima kutambua afya ya udongo kabla ya kutumia bidhaa zao ili kutumia bidhaa zinazoendana na aina ya virutubisho vinavyohitajika kwa mmea katika maeneo yao.

Aidha, aliwataka kutosita kueleza kero wanazokutana nazo kwenye shughuli zao za uzalishaji kwani, bodi ya wakurugenzi wakishirikiana na menejimenti ya TFRA kama wasimamizi wa tasnia wanaoweza kushauri namna bora ya kuendeleza na kutatua.

Naye, Mkurugenzi wa Uhamasishaji Uzalishaji wa Ndani na Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja, Josepy Charos alisema serikali ilitumia Sh. bilioni 700 kuagiza mbolea nje ya nchi ili kukidhi mahitaji ya wakulima nchini.



# Wizara ya Fedha yapewa siri ya kufanikisha Dira ya Maendeleo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WIZARA ya Fedha imeshauriwa kuwatumia wataalamu kufanya tathimini ya uhai wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2020/2050 ili kuhakikisha inaleta ufanisi.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Kanali Denis Mwile alitoa ushauri huo wakati akifungua mafunzo kuhusu dira hiyo kwa watumishi wa umma yaliyotolewa na Wizara ya Fedha.

Mafunzo hayo yaliwashirikisha watumishi mbalimbali wa umma wakiwemo wa taasisi za serikali, taasisi binafsi na viongozi wa dini wa Mkoa wa Mbeya.

Alisema, dira hiyo ni muhimu ikafahamika kwa Watanzania walio wengi ili kila mmoja anapofanya shughuli zake za uzalishaji ajipime na kutathimini maendeleo yake.

"Lakini pia ni vema maofisa uhusiano wakahamasishwa kutumia taaluma zao katika kuimarisha uhusiano na taasisi za maendeleo za kimataifa ili kuchochea dira yetu ifanikiwe," alisema Mwila.

Aidha, aliwataka washiriki waliohudhuria mafunzo hayo kutumia ujuzi walioupata kufikisha elimu kwa Watanzania wengine ili kupanua uelewa.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo walisema watahakikisha wanatumia mafunzo waliyoyapata kuwaelimisha wengine kuhusu maendeleo ya nchi na namna ya kushiriki kwenye maendeleo.

Mmoja wa washiriki hao, Juma Maduhu aliishukuru Wizara ya Fedha kwa kuamua kuwaelimisha kuhusu dira hiyo kwa maelezo kuwa asilimia kubwa ya Watanzania hawana uelewa kuhusu dira hiyo na faida zake.

Alisema kupitia mafunzo hayo watahakikisha wanawaelimisha watumishi wengine pamoja na Watanzania kupitia njia mbalimbali ikiwemo kwenye mikutano ya hadhara na vyombo vya Habari.

Alisema watatoa elimu kwa wananchi na kukusanya maoni yao kuhusu namna ya kuboresha dira hiyo,

Mchumi Mkuu wa Wizara ya Fedha, Alfred Missana alisema moja ya mafanikio ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ni pamoja na nchi ya Tanzania kufika uchumi wa kati wa chini mwaka 2020 na kwamba wataendelea kutoa elimu ili kuongeza uelewa.

Alisema mafunzo hayo yanafanyika nchi nzima kwa watumishi wa umma ambao pia watasaidia kuisambaza kwa Watanzania wengine kwenye maeneo husika.




Ofisa Udhibiti ubora wa mbolea wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Henrico Renatus (kushoto), akitoa elimu katika maonyesho ya wakulima, jijini Mbeya jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CCM yaagiza taasisi kuajiri makandarasi wenye sifa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, kimezitaka taasisi mbalimbali za umma mkoani humo kuhakikisha zinaajiri makandarasi wenye sifa ili miradi inayotekelezwa iwe na viwango na idumu muda mrefu.

Aidha, kimezitahadharisha taasisi zitakazoajiri makandarasi wasiokidhi viwango kuwa kitachukua hatua kwa kuwashtaki watendaji wake pamoja na kuwafukuza makandarasi husika kwenye miradi.

Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM walitoa angalizo hilo juzi wakati wa ziara ya kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ikiwa ni mwendelezo wa ziara katika wilaya zote.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Dk. Stephen Mwakajumilo alizitaja taasisi hizo kuwa ni Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) na mamlaka zinazohusika na miradi ya maji .

Alisema kumekuwa na tatizo la baadhi ya makandarasi wanaoajiriwa na taasisi hizo kutekeleza miradi chini ya kiwango na kusababisha iharibike ndani ya kipindi kifupi hali ambayo inaisababishia serikali hasara.

Alisema wakati wakiendelea na ziara wilayani Chunya walibaini mabomba yasiyokidhi viwango kutumika kwenye mradi wa maji wa Bwawa la Matwiga hali iliyosababisha wananchi kutofikiwa na huduma kutokana na mabomba hayo kupasuka.

Alisema chama hicho kitahakikisha makandarasi wa aina hiyo wanaondolewa ndani ya mkoa pamoja na kuwashughulikia wakuu wa taasisi hizo ili iwe fundisho. "Sisi hatutembelei miradi bali tunakagua, kumekuwa na tatizo kubwa la miradi ndani ya mkoa wetu kutekelezwa chini ya kiwango, ukienda pale Jiji kuna barabara zimetumia mabilioni lakini ndani ya kipindi kifupi zimefumuka, tutawafukuza makandarasi wa aina hiyo ndani ya mkoa wetu," alisema Dk. Mwakajumilo.

Alisema baadhi ya miradi hiyo huwa inachakachuliwa kwa ushirikiano kati ya makandarasi na baadhi ya viongozi wasiokuwa waaminifu.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC), Ndele Mwaselala anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, alisema serikali inaimarisha miundombinu ya barabara maeneo ya vijijini ili kufungua fursa za kiuchumi kwa wananchi.

Alisema barabara hiyo ya Inyala-Simambwe yenye urefu wa km. 16.7 itawasaidia wananchi wa kata za Tembela na Inyala kusafirisha mazao yao kwenda sokoni pamoja na kusafirisha pembejeo za kilimo.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya wanawake wa CCM (UWT) Mkoa wa Mbeya, Edna Mwaigomole alishauri mkandarasi anayejenga barabara hiyo kuboresha baadhi ya maeneo yenye matatizo.

Alisema kuna maeneo yanatakiwa kuwekwa njia na vivuko vya watembea kwa miguu kwenye maeneo ya makazi ya watu ili kueusha ajali.

Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza alisema barabara hiyo ni muhimu kwa wananchi kutokana na kata hiyo kuwa kinara wa uzalishaji wa mazao mbalimbali.

Alisema barabara hiyo ndiyo ya kwanza kujengwa kwa kiwango cha lami katika jimbo lake ambayo inapita maeneo ya vijijini na hivyo akawaomba viongozi wa chama kuendelea kushirikiana naye kuomba barabara zingine.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa alisema kwa mujibu wa mkataba mradi huo unatakiwa ukamilike kabla ya Oktoba Mosi mwaka huu.

# RC ahimiza wakulima kupewa kipaumbele

**Mwandishi Wetu,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera amesema wakulima wanapaswa kupewa kipaumbele ili nchi iweze kufikia malengo ya ajenda ya kuboresha sekta ya kilimo.

Amesema sekta ya a kilimo ndiyo inaajiri idadi kubwa ya Watanzania, hivyo wakulima wana nafasi kubwa katika kuchangia Pato la Taifa.

Aliyasema hayo jana wakati wa ufunguzi wa mkutano wa wakulima mkoani hapa ulioandaliwa na kampuni ya kutengeneza na kusambaza mbolea ya Yara Tanzania, kwamba zaidi ya wakulima 400 kutoka Nyanda za Juu Kusini walishiriki.

Akizungumza katika mkutano huo, Homera aliipongeza Kampuni ya Yara kwa kuthamini na kulifanya suala la kuwezesha wakulima wadogo kuwa kipaumbele.

Alisema serikali inatambua kuwa wakulima ni kundi muhimu zaidi katika kutimiza malengo ya kuifanya Tanzania kuwa kinara wa uzalishaji wa chakula Afrika.

"Kwa hivyo ninataka kuwashukuru Yara kwa juhudi zao za kumwinua mkulima. Na kama mwakilishi wa Serikali, niseme kwamba tutaipa Yara msaada unaohitajika ili kuharakisha mageuzi kupitia bidhaa zake bora za mbolea na huduma za kilimo," alisema Homera.

Alisema kituo cha maarifa cha Yara kilichofunguliwa hivi karibuni mjini Mbeya kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia (MUST) kitakuwa muhimu katika kampeni ya mageuzi ya kilimo.

Mkurugenzi Mkuu wa Yara Tanzania, Winstone Odhiambo, alisema ni wajibu wa Yara kuwawezesha wakulima wadogo kupata chakula cha kutosha na kuinua mamilioni ya watu kutoka katika umaskini kupitia uzalishaji wa kiwango cha juu cha kilimo, kuzalisha ajira kupitia mnyororo wa thamani.

"Tunatekeleza jukumu letu kwa kuzalisha mbolea tofauti na zenye ubora wa hali ya juu na virutubishi vingine vya mazao vilivyochanganywa ambavyo vinaongeza mavuno na hivyo kipato cha wakulima. Mtazamo wetu ulijumuisha suluhu za afya ya udongo, kilimo endelevu na ujenzi wa viwanda, ulinzi wa mazingira na kukabiliana na changamoto ya tabianchi". alisema.

Alisema maonesho ya Kilimo ya Yara yatakuwa yakifanyika kila mwaka kwa kampuni hiyo ili kuendeleza ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi na kuunga mkono ajenda ya Serikali ya maendeleo ya kiuchumi kupitia sekta ya kilimo ambayo ina nafasi kubwa zaidi kwa mamilioni ya Watanzania kufanikiwa.

## Zanzibar yafanikiwa kutokomeza malaria

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, alisema Zanzibar imepata mafanikio makubwa katika kutokomeza malaria.

Amesema mikakati ya serikali kuona ugonjwa huo hausababishi vifo vya kundi kubwa la jamii hasa wanawake na watoto. Pia amesema serikali imejipanga kutokomeza malaria na kuona kwamba si tishio tena kwa afya ya jamii.

Mazrui aliyasema hayo wakati aliposhiriki katika kampeni ya 'Tokomeza Malaria' kwa kugawa vyandarua vilivyowekwa dawa kuzuia mbu kumshambulia binadamu.

Mazrui alisema ugonjwa wa malaria bado upo licha ya juhudi kubwa za kupunguwa kasi yake iliokuwapo zamani. Katika kipindi cha mwaka 2023, vifo sita vimeripotiwa huku wagonjwa 3,747 wakigungulika na kupata matibabu.

Alisema kwa mujibu wa utafiti uliofanywa, vyandarua 247,660 vinahitajika katika kaya 78,443 na katika uzinduzi wa kampeni hiyo, wananchi 430,047 watanufaika na vyandarua hivyo.

''Ujumbe wangu malaria bado ipo licha ya juhudi zetu za kupambana na ugonjwa huo na kuona kwamba si tishio tena kwa afya za binadamu," alisema.

Aidha, aliwataka wananchi ambao watapata mgawo wa vyandarua hivyo katika awamu ya kwanza, kuvitumia vizuri kwa kuhakikisha watoto wanalala katika chandarua ambacho ndiyo njia salama ya kuepukana na ugonjwa huo.

Mwakilishi wa Shirika la Misaada la Marekani (USAID) anayeshughulikia masuala ya afya, Anna Hoffman, alisema wameridhishwa na juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupambana na malaria ambao matukio na takwimu za ugonjwa huo zimeshuka sana.

"USAID kwa kiasi kikubwa tunaridhishwa na juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kupambana na malaria," alisema.

Naye Meneja wa Kitengo cha Kupambana na Malaria Zanzibar, Shija Joseph Shija, alisema limekuwapo ongezeko la wagonjwa wa malaria na kutoa mfano katika mwaka 2023 kuanzia Januari hadi Juni, wagonjwa 3,563 waligundulika kulinganisha na mwaka 2022 ambapo wagonjwa 3,223 waligundulika.

Aliwataka wananchi kuhakikisha wanavitumia vyandarua hivyo ambayo vimewekwa dawa inayodumu kwa takriban miaka mitatu.

Aidha alisema kampeni hiyo itaendelea kufanyika kwa kuweka usafi katika maeneo ya mji ikiwemo katika madimbwi ya maji na kuona hakuna mazalia mapya ya mbu.

# Waziri ahimiza vijana kuchangamkia kilimo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, amewataka vijana kujikita katika kilimo ili kubadilisha maisha yao na kuachana na ndoto za kwenda Ulaya kutafuta kazi.

Amesema serikali katika bajeti yake imeongezwa kutoka Sh. Bilioni 53 mwaka 2022/23 hadi Sh. bilioni 98 mwaka 2023/24 kwa Wizara ya Kilimo ili kuiwezesha sekta hiyo kuwa tegemeo la kuzalisha ajira kwa vijana.

Shamata aliyasema hayo jana alipokabidhi vifaa mbalimbali vya usambazaji maji katika mashamba ya wakulima vyenye thamani ya Sh. milioni 47 katika mradi wa viungo unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU).

Alisema malengo ya serikali ya Zanzibar ya kuzalisha ajira 300,000 yatafikiwa na kwamba vijana wanayo nafasi kubwa ya kujiajiri katika kilimo cha mboga, matunda na viungo na kuingia katika sekta ya utalii kwa uhakika.

"Vijana huu si wakati tena wa kufikiria kwenda Ulaya kutafuta ajira. Ajira zipo hapa hapa katika sekta ya kilimo ambacho kinaweza kumkomboa mkulima na kupiga hatua kubwa ya Maisha," alisema.

Shamata alizipongeza asasi za kiraia zinazotekeleza mradi huo kwa kufanikiwa kuwashajihisha wakulima kujikita katika kilimo cha mboga matunda na viungo.

Alisema nia ya serikali ni kurudi katika enzi zake za miaka ya nyuma kuongoza katika uzalishaji wa mazao ya viungo na kusafirisha katika nchi za Ulaya na Asia hadi Uarabuni.

''Nachukuwa nafasi hii kwa dhati kuzipongeza asasi za kiraia ambazo zimeonyesha nia ya kuimarisha na kuwashajihisha wakulima kujikita katika kilimo cha viungo na mboga na hivyo kurudisha hadhi ya Zanzibar kuongoza kwa uzalishaji wa mazao hayo duniani," alisema.

Ofisa wa Mradi wa Viungo, Ali Said Juma, alisema mradi wa viungo tayari lengo lake kuwafikia wakulima 57,000 kwa njia mbalimbali hatua ambayo itaongeza thamani ya mnyororo wa bidhaa na uzalishaji wake.

Alisema kwa sasa tayari umewafikia wakulima 21,000 ambao hao wamepatiwa vifaa mbalimbali ikiwamo mbegu na vifaa vya usambazaji wa maji mashambani.

Naye Mkurugenzi wa Asasi ya Kiraia ya Pemba Forest ambayo ni sehemu ya utekelezaji wa mradi huo, Mbarouk Mussa Omar, alisema upatikanaji wa vifaa vya usambazaji wa maji mashambani kwa kiasi kikubwa utasaidia uzalishaji wa mazao na kuingia sokoni kwa mafanikio.

Miongoni mwa wakulima waliopata vifaa hivyo ikiwamo tangi la kuhifadhi maji kwa umwagiliaji mashambani, Mwatima Juma Ali, mkazi wa kijiji cha Umbuji wilaya ya Kati Unguja, alisema anajihusisha na kilimo cha mboga yakiwamo matikiti maji, bilinganyi na nyanya chungu na hifadhi ya maji na usambazaji wake ilikuwa miongoni mwa mahitaji yake makubwa.

Mradi wa viungo wa Agro-Connect unafadhiliwa na EU na kutekelezwa na asasi tatu za kiraia huku ukiwa na malengo ya kuimarisha kilimo cha mboga, matunda na viungo na kuimarisha masoko ya bidhaa kuingia sokoni kwa mafanikio makubwa.




Mshindi wa promosheni ya Cha Wote, Tausi Makoba (kulia), ambaye ni mfanyabiashara wa nguo za kike kutoka Makongo Juu, akipokea mfano wa hundi wa 1,000,000/- kutoka kwa Meneja wa Wateja Maalum wa Tigo Pesa, Mary Rutta jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ataka sera kuongoza wafungwa wanawake

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MHADHIRI Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU), Dk. Sikujuwa Omar Hassan, amesema wakati umefika kwa Chuo cha Mafunzo Zanzibar (Magereza) kuwa na sera itakayoweka wazi namna ya kuwaongoza wafungwa wanawake wanapokuwa katika maeneo hayo katika mazingira tofauti na kuleta ufanisi wa kazi.

Aliyasema hayo wakati akiwasilisha mada kwenye mafunzo yaliyowashirikisha maofisa na wapiganaji wanawake katika Chuo cha Mafunzo yaliyofanyika makao makuu ya chuo hicho, Kilimani, Unguja.

Dk. Sikujua alisema chuo hicho kipo sheria lakini tatizo kubwa hakina sera namna ya kuwaongoza wafungwa wanawake ambao wanakabiliwa na vifungo kutokana na ukiukwaji wa mambo mbalimbali ya sheria.

Alisema mikataba ya kimataifa na kikanda,na sera na sheria mbalimbali zimeelezea haki mbalimbali kwa wafungwa wakati wanapotumikia vifungo vyao magerezani.

''Wanafunzi wanawake wanaotumikia adhabu zao katika magereza wanahitaji mwongozo maalumu ambao utaweka bayana mahitaji yao pamoja na haki na fursa zingine," alisema.

Pia alisema wafungwa wa kike wanahitaji muongozo ambao utaweka bayana mahitaji yao zaidi pale wanapokabiliwa na kipindi cha ada zao za kila mwezi nguo za kujihifadhi.

Alisema wakati umefika sasa kuona sheria inayounda Chuo cha Mafunzo Namba 1 ya mwaka 1980 inawekwa bayana na kufahamika na maofisa na wapiganaji wote wanaofanya kazi katika vyuo vya mafunzo na kuitekeleza.

"Sheria inayounda vyuo vya mafunzo haifahamiki kwa kweli. Hata ukiitafuta katika mtandao haionekanai, sasa hili ni tatizo kubwa," alisema.

Kamishna Msaidizi wa Vyuo vya Mafunzo Zanzibar, Seif Maabad Ali, alisema wameomba kupatiwa mafunzo hayo kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ikiwamo kufanya kazi kwa kuzingatia sheria na utawala bora.

Alisema tayari katika vyuo vya mafunzo wameweka utaratibu wa kisanduku cha maoni ambacho wafungwa na mahabusu wako huru kutoa taarifa mbalimbali yakiwamo malalamiko.

Naye ofisa mwandamizi kutoka katika Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar anayeshughulikia ukatili wa kijinsia, Zaina Salum Abdalla, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha watendaji wa vyuo vya mafunzo kwenda sambamba na mikakati ya kupambana na udhalilishaji wa kijinsia na kuimarisha utawala bora.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA UBUNGO**
**LILILOPO KIBAMBA – LUGURUNI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA 72 YA MWAKA 2023**
**ISRAEL SIMBA & 3.......................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**GEORGE MASHAKA CHIMALILO................WAJIBU MAOMBI**
**KUITWA SHAURINI**

**GEORGE MASHAKA CHIMALILO - POPOTE ULIPO**

**ISRAEL SIMBA & 3**
Amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) UBUNGO lililopo Luguruni/Kibamba Maombi hayo yamepangwa kutajwa tarehe 15/8/2023 saa 8:30. Hivyo basi unatakiwa wewe mwenyewe au Wakili wako kuleta utetezi wako ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya tangazo hili kutolewa. Vielelezo vyote vinavyohusu shauri tajwa vinapatikana katika Masijala ya wazi wa Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Ubungo. Endapo hamtatekeleza/hautatekeleza maombi haya yatasikilizwa upande mmoja na uamuzi/amri kutolewa.
Imetolewa na kutiwa muhuri wa Baraza leo tarehe 20/7/2023

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
(W) – UBUNGO
DAR ES SALAAM

## KUPOTELEWA KWA CHETI




**ROSE AMBROSE MINJA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index No. S0389-0043 kilichotolewa na baraza la mtihani kupitia SHAURITANGA SEC. SHOOL Mwaka 2015. Yeyote atakaekiona atoe taaria kituo cha polisi. Taarifa ya polisi. **MWA/NYA/RB/247907/2023.**

## KUPOTELEWA KWA CHETI



**ROSE AMBROSE MINJA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha Sita chenye index No. S0389-0510 kilichotolewa na baraza la mtihani kupitia SHAURITANGA SEC. SHOOL Mwaka 2018. Yeyote atakaekiona atoe taaria kituo cha polisi. Taarifa ya polisi **MWA/NYA/RB/247902/2023.**

## KUPOTELEWA KWA CHETI



**BARAKA FRANCIS JOHN** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.1686/0050 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia KEMORAMBA SEKONDARI mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MWA/MAG/RB/238599/202**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

LYDIA THECLA BOMA anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya LANDCRUISER HARDTOP yenye usajili namba: T255 ADQ. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: MTW/NEW/RB/241284/2023

## KUPOTELEWA NA CHETI



**SHARON RICHARD GWAU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.4967/0075** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia ST. ALOYSIOUS SEKONDARI mwaka 2020. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CHU/RB/247463/2023.**

## TANGAZO LA KUPOTEA NYARAKA YA UMILIKI WA KIWANJA

Wilfred Tune ambaye ni msimamizi wa mirathi ya marehemu Agata saidi.

Atangaza kupotelewa na nyaraka ya umiliki wa kiwanja namba 142 kitalu "Y-1" kilichopo Ibanzamata Manispaa ya Shinyanga.

Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Wilfred kwa simu namba 0789-498783.

**Taarifa ya Polisi namba ya malipo 9910829962804/2021.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA CHAMWINO**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......31/2009**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: AMANI ALLY wa MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA ASHA AMANI ALLY**

**TANGAZO**
(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 04 Mwezi 08 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 21 mwezi 07 mwaka 2023

2023
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO
MOROGORO

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

HILDEGADA MGAYA anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba ya usajili MC 154 DHB AINA YA KINGLION. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya polisi: IRI/IRI/RB/248936/2023.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

KINGLION INVESTMENT CO. LIMITED INATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI ZA PIKIPIKI ZENYE NAMBA ZA USAJILI MC 680 DDD na MC 101 CZD AINA KINGLION. YEYOTE ATAKAYEZIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA ZA POLISI: IRI/IRI/RB/249032/2023; IRI/IRI/RB/249030/2023.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA KWIMBA NGUDU**
**RUFAA YA MADAI/JINAI NA 10 MWAKA 2023**
**(KUTOKA MAHAKAMA YA MWANZO BUYOGO WILAYA YA KWIMBA)**
**ENOCK MASELE NYANDA..........MDAI**
**DHIDI YA**
**BAYPORT FINANCIAL SERVICES LIMITED......MDAIWA**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA : BAYPORT FINANCIAL SERVICES LIMITED**
MAHAKAMA HII INAKUFAHAMISHA KWAMBA MDAI AMEFUNGUA SHAURI LA RUFAA DHIDI YAKO.
RUFAA IMEPANGWA KUSIKILIZWA MNAMO TAREHE 01/08/2023 SIKU YA JUMANNE SAA 2:30 ASUBUHI NA UNATAKIWA KUWEPO, AU KUWAKILISHWA KISHERIA PAMOJA NA KULETA UTETEZI WAKO DHIDI YA MADAI HAYO.
IMETOLEWA KWA AMRI YANGU NA MHURI WA MAHAKAMA HII LEO 17/07/2023

MAHAKAMA YA (W)
KWIMBA.

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE DISTRICT COURT OF MVOMERO**
**AT MVOMERO**
**CRIMINAL/CIVIL CASE NO.02/2023**
**SEMBUKA KIPALA .........PLAINTIFF**
**VERSUS**
**1. RAMADHAN ZUBERI RAMADHAN..... DEFENDANT**
**2. RAMJAAN MEAT LIMTED......DEFENDANT**

**NOTICE OF DATE MENTION/HEARING**

THE NOTICE that the above case has been fixed for Mention/Hearing on 28 day of 07 2023 at 9:00 a.m before Hon. A.H. WAZIRI DRM
YOUR ARE require to appear in this Court without fail and you must produce to that day all the documents upon which you intend to reply in support of your case.
GIVEN under my hand and the seal of the Court this 20 day of 07 2023.

DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE
MVOMERO

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701*

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0677020701
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,
WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Polisi wanawake wanolewa kukabili uhalifu wa kimataifa

**Na Renatha Msungu**

KAMISHNA wa Jeshi la Polisi Zimbabwe, Grace Ndou, amesema Mafunzo ya Jumuiya ya Askari Wanawake wa Jeshi la Polisi kutoka Ukanda wa Afrika (IAWP), yatawasaidia kwa kiasi kikubwa kufungua mipaka ya kupambana na uhalifu unaovuka mipaka katika maeneo mbalimbali.

Mbali na hilo, amesema mafunzo hayo yatazidi kuongeza ushirikiano baina ya askari kutoka nchi mbalimbali, ikiwamo kupeana mbinu za kukabiliana na uhalifu katika maeneo ya mipaka husika.

Kamishna Ndou aliyasema hayo jana baada ya kuhudhuria mafunzo ya Jumuiya ya Askari Wanawake wa Afrika yanayoendelea jijini Dar es Salaam, yakishirikisha askari hao kutoka nchi mbalimbali za Afrika.

Alisema mada zilizofundishwa katika mafunzo hayo zimesaidia kupanua wigo wa utendaji kazi za kila siku, hususani katika masuala ya kupambana na uhalifu katika maeneo ya mipaka inayozizunguka nchi wanazofanya kazi.

"Tunashukuru kwa kupata mafunzo haya, ninaamini baada ya mafunzo kila askari wa kike aliyeshiriki mafunzo hayo ataondoka na ujuzi wa kwenda kutumia kazini," alisema Kamishna Ndou.

Mbali na hilo, alisema mafunzo hayo pia yatawasaidia kuwajengea uhusiano mzuri askari hao katika utendaji kazi na vyombo vingine vya ulinzi na usalama na kuongeza kuwa hiyo ni hatua kubwa kwa Jeshi la Polisi.

Mrakibu Mwandamizi wa Jeshi la Polisi nchini, Georgina Matagi, alisema mafunzo hayo yamewajengea ufahamu zaidi askari katika masuala ya ukatili wa kijinsia, rushwa na namna ya kufanya kazi na jamii.

Aliwashukuru waandaaji wa mafunzo hayo ambayo anaamini yanakwenda kuleta mabadiliko katika utendaji kazi wao wa kila siku katika vituo vyao vya kazi ambavyo wanawajibika kiutendaji.

Sajenti wa Polisi, Mwanema Salehe kutoka Arusha, alisema mafunzo hayo yamekuja wakati mwafaka hasa ukizingatia kuna wimbi la uhalifu mbalimbali unaojitokeza katika maeneo mbalimbali.

Mafunzo hayo yalianza kwa kongamano ambalo lilifunguliwa mwishoni mwa wiki na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, katika Uwanja wa Uhuru, mkoani Dar es Salaam.

# Jela miaka miwili kwa kumiliki mimea ya dawa za kulevya

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam imewahukumu kifungo cha miaka miwili jela Schola Kashinde na James Mayunga, baada ya kukiri kumiliki mimea isiyokubalika aina ya bangi kilogramu 59.59 kinyume cha sheria.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mkuu, Mary Mrio wa mahakama hiyo baada ya washtakiwa hao kutimiza masharti ya makubaliano waliyoingia na Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) ya kuhukumiwa kifungo hicho.

Kabla ya kusoma hukumu hiyo, Hakimu Mrio aliutaka upande wa mashtaka uwakumbushe washtakiwa mashtaka yanayowakabili pamoja na makubaliano waliyoingia na DPP.

Baada ya kusomewa mashtaka yao, washtakiwa wote walikiri kutenda kosa hilo.

Hakimu Mrio alisema mahakama inawatia hatiani baada ya kukiri makosa yao ya kukutwa na mimea isiyoruhusiwa aina ya bangi kinyume cha Sheria na pia kwa kuzingatia makubaliano yao na DPP, anawahukumu kifungo cha miaka miwili jela.

Katika kesi hiyo, washtakiwa hao walikuwa wanakabiliwa na mashtaka ya kukutwa na mimea isiyoruhusiwa aina ya bangi kilogramu 59.59.

Inadaiwa kuwa Machi 12, 2019, eneo la Kindamba, Wilaya ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam, washtakiwa walikutwa wakimiliki mimea isiyoruhusiwa aina ya bangi yenye uzito wa kilogramu 59.59.



Meneja wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB), Dk. Jaspa Samweli, akionyesha kwa waandishi wa habari, mjini Iringa jana, mifuko iliyojaa uchafu mbalimbali wa mahindi ya wakulima yaliyochambuliwa baada ya kuuzwa. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# SBL yatumia bil. 12/- kwa wakulima wadogo

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Serengeti Breweries Limited (SBL) imebainisha kutumia Sh. bilioni 12 kwa jamii za Watanzania katika kununua nafaka mwaka wa fedha uliopita, huku ikiweka mikakati ya kushirikiana na wakulima wadogo wengi zaidi wilayani Handeni mkoani Tanga.

Vilevile, kampuni hiyo imeanza kuandikisha wakulima wilayani humo kuanza kulima mtama ambao kampuni hiyo itanunua kwa ajili ya uzalishaji.

Katika mradi huo ambao unatarajiwa kuanza mwakani, SBL itakuwa na jumla ya mikoa minane ambayo inachukua malighafi zake, huku ikiwa na mipango ya kuongeza mikoa mingine ikiwamo Mbeya na Kagera.

Kwa sasa, SBL inapata malighafi zake kutoka mikoa saba ya Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Dodoma, Iringa, Singida na Shinyanga.

Kama sehemu ya maandalizi ya awali ya mradi huo, wakulima wilayani Handeni tayari wameanza kusajiliwa kushiriki katika mradi huo huku ekari 658 za ardhi zikitengwa kwa ajili ya mradi ambao utajumuisha mashamba ya majaribio.

Mradi huo unatarajiwa kuleta manufaa kwa wakulima wa Handeni kwa kuzingatia kipaumbele kutolewa kwa wanawake na vijana. Ni mradi utakaoimarisha zaidi azma ya SBL ya kuongeza ukusanyaji wa malighafi zake kutoka kwa wakulima wadogo hadi kufikia asilimia 85, ambayo ni sawa na tani 13,000 ifikapo mwaka 2024 kutoka asilimia 70 ya sasa, ambayo ni sawa na tani 11,000.

Uwekezaji wa SBL kwa wakulima wadogo ni sehemu ya nguzo muhimu ya kampuni hiyo inayojulikana kama 'Kutoka Nafaka hadi Glasi'. Katika kutekeleza nguzo hiyo, SBL inashirikiana kwa karibu na wakulima wadogo si tu kupata malighafi kutoka kwao, bali pia kuwawezesha kiuchumi.

"Hadi sasa tumeshirikisha jumla ya wakulima 400 katika mikoa saba ambapo tayari tuna kanzidata ya wakulima tunavyofanya nao kazi, Kwa mfano, katika mwaka wa fedha uliopita tumenunua jumla ya tani 11,000 za malighafi yetu kutoka kwa wakulima wadogo katika mikoa saba ambayo tayari iko kwenye kanzidata yetu.

"Hili ni ongezeko la asilimia 70 kulinganishwa na asilimia 65 ambayo tulipata kutoka kwao mwaka wa fedha uliopita," alisema Meneja wa Mawasiliano na Uendelevu wa SBL, Rispa Hatibu.

Akizungumzia mradi wa kilimo cha mtama uliokusudiwa katika Wilaya ya Handeni, Hatibu alisema SBL imekuwa inafanya kazi kwa karibu na Ofisa Kilimo wa Wilaya, Yibarila Kamele, kutambua maeneo yanayofaa kwa mradi huo pamoja na kuwasajili wakulima wadogo wa Handeni ili washiriki katika mradi huo wa kilimo cha mtama.

Kamele alisema: "Awali tulikuwa tumepanga wakulima waanze kulima mwaka huu lakini tukaona kwamba msimu huu hautotupatia matokeo bora. Kwa hiyo, nilipendekeza utekelezaji wa mradi uanze mapema mwaka ujao, hii itawapa wakulima nafasi ya kuandaa mashamba yao vizuri kwa ajili ya mradi huu."

Hatibu alisema kampuni hiyo inatarajia kuongeza idadi ya wakulima wadogo kutoka 400 wa sasa hadi 700 ifikapo mwaka 2025, ambapo kutahusisha kuongeza mikoa zaidi ikiwa ni pamoja na Tanga, Mbeya na Kagera.

# STRAIKA MCAMEROON KUTUA YANGA KESHO

**Na Saada Akida**

MABOSI wa Yanga wamefanikiwa kukamilisha usajili wa mfungaji bora wa Ligi Kuu ya Cameroon, Emmanuel Dikongue, kwa mkataba wa miaka miwili kwa ajili ya kuziba pengo la mshambuliaji anayeondoka Yanga, Fiston Mayele.

Dikongue, (28) anatarajia kutua nchini kesho akiwa anajiunga na Yanga akitokea Klabu ya Canon Yaounde ya Cameroon, ambapo kabla ya hapo aliichezea Akonangui FC ya Equatorial Guinea.

Taarifa za uhakika zilizolifikia Nipashe jana kutoka ndani ya Yanga, zimeeleza kuwa Dikongue anakuja Yanga kuziba pengo la Mayele ambaye muda wowote kibao cha kuagwa kitaonekana mitandaoni, akielekea kujiunga na Pyramids ya Misri.

"Ni kweli, uongozi umekamilisha usajili wa mshambuliaji kutoka Cameroon anayekuja kuchukua nafasi ya Mayele ambaye hakuwapo hata katika utambulisho wa juzi kwenye Tamasha la Kilele cha Siku ya Mwananchi."

"Nadhani wakati wowote watamtangaza kwa sababu kila kitu kimeshakamilika juu yake hasa upande wa mkataba, kinachosubiriwa ni kuwasili kwake kwa ajili ya kumtangaza kabla ya kuanza kwa ligi na mechi za Ngao ya Jamii," alisema mtoa taarifa wetu.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ally Kamwe, alisema mchakato wa usajili unaendelea baada ya Kocha Miguel Angel Gamond kuona wapi anatakiwa kuongeza nguvu baada ya mechi yao ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini.

Alisema usajili unaendelea na bado kuna nafasi moja ya mchezaji wa kigeni ambapo mchakato huo unafanywa na rais wao, Hersi Said, ili kuimarisha timu yao kuelekea msimu mpya.

"Tumeona wachezaji wapya tuliosajili na sasa bado nafasi moja ya mchezaji wa kigeni ambaye taratibu za usajili zinaendelea kukamilika kwa kushirikiana vizuri na Kocha Gamond (Miguel Angel)," alisema Kamwe.

ITAKUWA HIVI...



Meneja Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu uzinduzi wa wiki ya Tamasha la Simba Day. **MPIGAPICHA WETU**

## Shikangwa wa Simba Queens atimkia China

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA namba moja wa Timu ya Soka ya Wanawake ya Simba, (Simba Queens) na mfungaji bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Jentrix Shikangwa, amejiunga na Klabu ya Beijing Beikong Women ya nchini China.

Straika huyo ambaye alipachika mabao 17 akiwa amesajiliwa kipindi cha dirisha dogo la usajili, amejiunga na klabu hiyo baada ya kumaliza mkataba wake na Simba Queens, huku akiwa amesaini mkataba wa miezi sita na klabu yake hiyo mpya.

Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo imeeleza kuwa hawatokuwa na mchezaji huyo kuelekea msimu ujao wa mashindano yanayowakabili.

"Mshambuliaji kinara, Jentrix Shikangwa, hatutakuwa naye msimu ujao baada ya mkataba wake kumalizika," ilieleza taarifa hiyo ya Simba.

Habari kutoka kwa baadhi ya vyombo vya habari nchini Kenya, zimeeleza kuwa straika huyo anayeichezea Timu ya Taifa ya Kenya kwa Wanawake 'The Harambee Starlets', baada ya kumaliza mkataba wake, alikuwa anawindwa na klabu mbalimbali zikiwamo Mamelodi Sundowns na Yanga Princess, lakini mwisho wa siku alikubaliana na dili la klabu hiyo ya Ligi Kuu nchini China ambalo lilikuwa nono zaidi.

Straika huyo mwenye nguvu na mashuti makali, aliwaaga na kuwashukuru mashabiki wa Simba Queens kwenye mtandao wake wa kijamii wa Instagram.

"Nashukuru Simba Queens na mashabiki wote kwa upendo wenu na sapoti yenu kwangu, ngoja tujaribu tena sehemu nyingine," alisema mchezaji huyo ambaye pamoja na kwamba hakuipa timu hiyo ubingwa, lakini aliiwezesha kumaliza nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu msimu uliomalizika.

Shikangwa ndiye alionekana kuchukua kijiti cha straika Mtanzania Opa Clement kwenye ufungaji ndani ya kikosi hicho ambaye naye aliondoka Machi mwaka huu kwenda kucheza soka la kulipwa nchini Uturuki kwenye Klabu ya Besiktas.

## Pluijm afurahishwa viwango Singida FG

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la Klabu ya Singida Fountain Gate FC, limeeleza kufurahishwa na kiwango kilichooneshwa na wachezaji wake kwenye mchezo wa kirafiki walioucheza hapo juzi dhidi ya Namungo FC na kuibuka na ushindi wa mabao 2-0.

Akizungumzia mchezo huo, Karatu mkoani Arusha, Kocha Mkuu wa Singida Fountain Gate, Hans van Pluijm, alisema wachezaji wake wameonesha kile anachokihitaji na kudai wameanza kuwa na muunganiko mzuri.

"Ninawapongeza wachezaji wangu wamefuata maelekezo niliyowapa tumefanikiwa kutoka na ushindi, hii ni ishara nzuri kuelekea mchezo wetu wa Ngao ya Jamii utakaotukutanisha na timu ya Simba," alisema Pluijm.

Alisema mchezo ulikuwa mgumu na wenye upinzani mkubwa kwani kila timu ilicheza vizuri kutokana na usajili zilizofanya.

Kwa upande wa Msemaji wa timu hiyo, Hussein Masanza, alisema maandalizi kuelekea Siku ya Singida (Singida Big Day), inayotarajiwa kufanyika Agosti 2, mwaka huu, yanaendelea vema na kwamba wataitumia siku hiyo kutangaza wachezaji wao ambao wamewasajili msimu huu.

## Prisons kujipima na Songwe Kombaini

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha Timu ya Tanzania Prisons chenye maskani jijini Mbeya, leo kinatarajiwa kucheza mchezo wa kirafiki na timu ya Kombaini ya mkoani Songwe, imeelezwa.

Akizungumza na Nipashe jana kutoka jijini Mbeya, Msemaji wa timu hiyo, Jackson Mwafulango, alisema mchezo huo ni mwendelezo wa michezo yao ya kirafiki ikiwa ni maandalizi ya kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara unaotarajiwa kuanza Agosti 15, mwaka huu.

"Mchezo huo ni maandalizi kuelekea msimu ujao ambao tunaamini utakuwa na ushindani mkubwa kutokana na usajili uliofanywa na timu zote," alisema Mwafulango.

Alisema Jumapili ya wiki hii atatoa taarifa rasmi ya wapi wanakwenda kuweka kambi yao ili mashabiki pamoja na wadau wa Prisons wafahamu kile kinachoendelea.

Wakati huo huo, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Fred Felix Minziro, amesema maandalizi yanaendelea vema kwa ajili ya mchezo huo utakaopigwa Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**HOJLUND NA MAN UTD**
KLABU ya Manchester United iko tayari kuwasilisha ofa rasmi kwa Atalanta kwa ajili ya kumnunua mshambuliaji wa Denmark, Rasmus Hojlund mwenye umri wa miaka 20, wiki hii. **(Mail)**

**CAICEDO BADO CHELSEA**
JARIBIO la Chelsea kumsajili kiungo wa kati wa Ecuador, Moises Caicedo mwenye umri wa miaka 21 kutoka Brighton limekwama. **(Guardian)**

**UNITED YATAKA NYOTA**
MANCHESTER United inamfuatilia mshambuliaji wa Eintracht Frankfurt mwenye umri wa miaka 24, Mfaransa Randal Kolo Muani, na kocha Erik ten Hag anavutiwa na mshambuliaji mwingine wa Ajax, Mghana Mohammed Kudus (22), ambaye amekuwa akihusishwa na Chelsea. **(Mirror)**

**PSG KUJIKITA KWA KANE**
IKIWA Kylian Mbappe atahamia Saudi Arabia basi PSG itafikia thamani ya fedha inayotaka Tottenham ya pauni milioni 100 kwa ajili ya mshambuliaji, Harry Kane mwenye umri wa miaka 29, ingawa Bayern Munich bado wana imani na nahodha huyo wa England kuwa atachagua kwenda Ujerumani. **(Independent)**

**TEN HAG AMTAKA KIPA**
KOCHA Erik Ten Hag pia anatarajia kuimarisha safu yake ya ulinzi kwa kusajili golikipa wa akiba wa timu yake. Anamtaka mchezaji wa kimataifa wa Uturuki anayecheza Fenerbahce, Altay Bayindir, 25. **(Goal)**

**MBAPPE AGOMBEWA EPL**
KLABU za Chelsea, Manchester United na Tottenham Hotspur zitakuwa sehemu ya shamrashamra za kutaka kumnunua mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 24, baada ya Paris St-Germain kupokea ofa ya rekodi ya dunia ya pauni milioni 259 kutoka kwa Al-Hilal ya Saudi Arabia ili kumnunua mchezaji huyo. **(Telegraph)**

**HENDERSON AAGA LIVER**
KIUNGO wa kati wa England, Jordan Henderson mwenye umri wa miaka 33, amewaaga wafanyakazi na wachezaji wenzake katika Klabu ya Liverpool kabla ya uhamisho wake wa kujiunga na Klabu ya Saudia ya Al-Ettifaq kukamilishwa. **(Mail)**

**HILAL YAKOMAA NA MBAPPE**
KLABU ya Al Hilal inapanga kumpa Kylian Mbappe mshahara wa jumla ya euro milioni 200 kwa mwaka huku wakimruhusu kuwa na asilimia 100 ya haki zake zote za picha kwenye matangazo. **(Fabrizio Romano)**

**TOURE AWINDWA EVERTON**
KLABU ya Everton inakaribia kumnasa mshambuliaji wa Almeria, El Bilal Toure mwenye umri wa miaka 21, licha ya ushindani kutoka kwa Klabu ya Atalanta inayomtaka pia mchezaji huyo wa Kimataifa wa Mali. **(Football Insider)**

**BARCA YAJITOA KWA MBAPPE**
KLABU ya Barcelona wamejiweka kando kwenye sakata la kumnunua Kylian Mbappe licha ya madai kuwa walifanya mazungumzo na PSG. **(Marca)**

**MITROVIC ATAKIWA SAUDIA**
KLABU ya Saudi Arabia Al Hilal inakaribia kufikia makubaliano na Fulham ya kumsajili mshambuliaji wa Serbia, Aleksandar Mitrovic mwenye umri wa miaka 28. **(90min)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE AIGOMEA PSG KUSAJILIWA SAUDI ARABIA

## Kwa sasa yupo tayari kukaa benchi msimu mzima ili kumalizia mkataba wake, kisha...

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe hana nia ya kucheza Saudi Arabia licha ya Paris Saint-Germain kuipa Al-Hilal ruhusa ya kuzungumza na nyota huyo wa Ufaransa baada ya kuweka mezani dau la rekodi ya dunia la pauni milioni 259.

Mbappe anauzwa na mabingwa hao wa Ufaransa baada ya kukataa kusaini mkataba mpya ukiwa umesalia mwaka mmoja kumalizika.

Habari za ofa hiyo zilikuja mapema Jumatatu na PSG walikuwa na uwezekano wa kukubali kama rais Nasser Al-Khelaifi hana nia ya kumpoteza bure katika msimu ujao wa majira ya joto.

Relevo iliripoti kwamba Mbappe 'hataki kucheza Saudi Arabia' licha ya ofa nzuri ya Al-Hilal.

Taarifa kutoka Madrid zinadai Mbappe amedhamiria kumaliza mwaka wa mwisho wa mkataba wake na mabingwa hao watetezi wa Ufaransa.

Mbappe anaripotiwa kuwa 'tayari kukaa benchi msimu mzima' huku akimalizia mpango wake'.

Msimamo huo umekuwa changamoto kubwa kwa kocha mpya wa PSG, Luis Enrique.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 tayari alikuwa ameachwa nje ya ziara ya PSG ya kujiandaa na msimu mpya nchini Japan na Korea Kusini, huku mustakabali wake ukiumiza kichwa.

Ofa ya Al-Hilal ingefunika uhamisho wa Neymar wa pauni milioni 198 kutoka Barcelona kwenda PSG kama uhamisho ghali zaidi katika historia ya soka.

Ofa iliyopo mezani inasemekana itamfanya Mbappe kupata pauni milioni 600 ndani ya mwaka mmoja pekee.

Inadaiwa kuwa klabu hiyo ya Saudia Pro League inaweza kuweka kipengele cha kutolewa katika mkataba mnono ambao unaweza kumruhusu Mbappe kusaini Real Madrid msimu ujao wa majira ya joto.

Nyota huyo wa Ufaransa kwa muda mrefu amekuwa akitamani kuhamia Real Madrid, huku PSG wakiamini kuwa tayari amekubali kujiunga na wababe hao wa Hispania bila malipo mwaka 2024.

Mbappe hapo awali alikaribia kujiunga na kikosi cha Carlo Ancelotti mwaka 2022, kabla ya kuamua kubaki PSG.

# HODGSON ASIKITIKA KUMPOTEZA ZAHA



**LONDON, England**

KOCHA Roy Hodgson amesikitika kumpoteza mtu mahiri katika Klabu ya Crystal Palace baada ya Wilfried Zaha kuihama na kujiunga na miamba ya Uturuki, Galatasaray.

Zaha, alikuwa mchezaji huru baada ya kumalizika kwa mkataba wake na Crystal Palace na alifichua kuwa alikuwa Istanbul kwa mazungumzo, baada ya kuripotiwa kukataa ofa ya mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki ya kusalia pale Selhurst Park.

Mapema wiki hii, alitumia Instagram kuthibitisha kuondoka kwake Palace, klabu ambayo alijiunga nayo akiwa na umri wa miaka 12 na kufunga mabao 90 katika mechi 458, akielezea jezi yao kama "ngozi yake ya pili".

Baada ya Galatasaray kutangaza kuwa Zaha amesaini mkataba wa miaka mitatu wenye thamani ya pauni milioni 3.75 kwa mwaka, Hodgson alionesha kusikitishwa kwake na kuondoka kwa mshambuliaji huyo.

Hodgson alisema, "Nilihuzunika sana kusikia kwamba Wilf ameamua kuondoka na kuanza ukurasa mpya katika maisha yake ya soka. Siku zote nilikuwa na matumaini kwamba angeweka mustakabali wake kwa klabu na ningekuwa na manufaa ya kufanya naye kazi tena msimu huu."

Kocha huyo amesema kuwa angependa kumshukuru yeye binafsi kwa yote aliyofanya wakati wake kama kocha.

"Klabu inapoteza mtu mashuhuri na, ingawa tunasikitika kwamba haikuwezekana kumshawishi Wilfried kukaa muda mrefu, tunaweza tu kumtakia kila la heri yeye na familia yake katika mradi wao mpya," alisema kocha huyo.

Zaha aliondoka Palace na kujiunga na Manchester United mwaka 2013, lakini alirejea London kwa mkopo mara mbili kabla ya kurejea rasmi mwaka 2015.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ivory Coast, ambaye aliichezea England mara mbili kabla ya kubadili uraia wake, pia alikuwa akihusishwa na Lazio, Fenerbahce na Al-Nassr msimu huu wa majira ya joto.

# Suarez kumfuata Messi Marekani

**SAO PAULO, Brazil**

MCHEZAJI wa zamani wa Brazil, Liverpool na Gremio Lukas Leiva anaamini Luis Suarez atamfuata Lionel Messi, Sergio Busquets na Jordi Alba kule Inter Miami.

Nyota huyo wa Liverpool na Barcelona, Suarez, alijiunga na Gremio Januari, baada ya kuisaidia klabu yake ya utotoni Nacional kutwaa taji la Ligi Kuu ya Uruguay aliporejea Amerika Kusini mwaka jana.

Suarez amefunga mabao manne katika mechi 12 kwenye Ligi Kuu ya Brazil msimu huu, lakini mustakabali wake uko shakani huku kukiwa na ripoti kwamba ndiye anayelengwa na Miami.

Miami tayari imewasajili wachezaji wenza wa Suarez wa zamani wa Barca, Messi, Busquets na Alba.

Hatua hiyo imeongeza uvumi kuhusu uhamisho wa Suarez, na ingawa Lucas anaelewa matokeo ya MLS, anatumai Gremio inaweza kumbakisha mshambuliaji huyo.

Alipoulizwa kuhusu mustakabali wa Suarez, Lucas ambaye alistaafu Machi




baada ya kugundulika kuwa na tatizo la moyo, alisema: "Alifanya kazi nzuri sana hapa Brazil akiwa Gremio. Nadhani alifanya hatua sahihi. Luis ni mchezaji wa kiwango cha dunia, hatuhitaji kuzungumzia sifa zake na kile anachofanya hapa Brazil. Amehusishwa, lakini natumaini anaweza kubaki Gremio kwa sababu ni klabu yangu na ni jirani yangu hapa."

Anatumai atasalia kwa muda mrefu, lakini MLS inapata uangalizi kutoka kwa kila mchezaji na mashabiki.

Baada ya Messi kuashiria mechi yake ya kwanza Miami kwa bao la ushindi wa 'frikiki' dhidi ya Cruz Azul kwenye Kombe la Ligi, bila shaka hakujawa na wakati mzuri zaidi wa kufuata MLS.

Lucas ni miongoni mwa waliofurahishwa na uwezo wa ligi, akiongeza kuwa MLS inakua kila mwaka, na watu wanatazama zaidi ligi hiyo.

"Tunaweza kumuona kwenye ligi nyingine, si Ulaya. Marekani, ni jambo zuri kwa mashabiki wanaopenda soka. Ni ligi ambayo inaimarika na inakua na kuwa bora kila msimu."

# Pochettino akunwa na Colwill

**LONDON, England**

KOCHA wa Chelsea, Mauricio Pochettino, anaamini Levi Colwill anaweza kuwa mmoja wa mabeki wa kati wakubwa nchini England baada ya mchezo wake mzuri wa kujiandaa na msimu dhidi ya Brighton.

Beki huyo mwenye miaka 20, alicheza dakika 81 za ushindi wa 'The Blues' wa 4-3 dhidi ya Seagulls katika mechi ya ufunguzi wa Msururu wa Ligi Kuu.

Colwill alitumia msimu uliopita kwa mkopo kule Brighton, ambapo alicheza mechi 22 katika mashindano yote na kuongeza sifa yake kama mmoja wa watu wanaotarajiwa kuimarika zaidi katika taifa lake.

Beki huyo pia aliisaidia Timu ya Taifa ya Vijana ya England kutwaa ubingwa wa Ulaya kwa vijana chini ya umri wa miaka 21.

Alipotakiwa kutoa mawazo yake kuhusu Colwill baada ya ushindi kwenye Uwanja wa Lincoln Financial, Pochettino alisema: "Levi amekuwa na siku chache mazoezini na nadhani yuko karibu kuwa fiti. Kwa kweli, kwa nini tunacheza naye ni kwa sababu tunahitaji kugawana dakika na wachezaji tofauti na nadhani yuko katika hali nzuri."

"Nimefurahishwa naye, uchezaji wake ulikuwa mzuri. Bora kuliko nilivyotarajia kwa sababu ni mechi ya kwanza tu kwetu baada ya msimu na Brighton," alisema Pochettino.

Colwill alijiunga na Chelsea mwaka 2011 na ameendelea kupitia mfumo wa vijana wa klabu hiyo, ingawa bado hajaonekana kwenye kikosi cha kwanza katika mechi ya ushindani.

Amecheza mara 26 kwenye kikosi cha vijana chini ya umri wa miaka 21, akifunga mara moja dhidi ya Manchester City.

Lakini baada ya Kalidou Koulibaly kuondoka Stamford Bridge na Wesley Fofana na Benoit Badiashile wote wakiwa wamejeruhiwa, mchezaji huyo wa zamani wa Huddersfield sasa anaonekana kuwa tayari kucheza mara kwa mara pamoja na beki mkongwe wa kati, Thiago Silva.



HABARI MICHEZO

# ROBERTINHO APAGAWA NA VIWANGO NYOTA WAPYA

Na Adam Fungamwango

BAADA ya sare ya bao 1-1 juzi dhidi ya timu ya Ligi Kuu ya Azerbaijani, Zira FC, Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira ameonesha kufurahishwa na viwango vya wachezaji wake hasa wapya iliyowasajili msimu huu, akisema safari hii ana kikosi kipana na hatopata tabu kwenye 'sub' ama kukiwa na majeruhi.

Akizungumza baada ya mechi hiyo kumalizika nchini Uturuki juzi ambapo inajiandaa na msimu mpya, kocha huyo raia wa Brazil ambaye alikishuhudia kikosi chake akiwa ndiyo kwanza amefika kutoka nchini Brazil alikokwenda kwa ajili ya kozi fupi, alisema anaona sasa viwango vya wachezaji wake vinawiana kwa anayeingia na anayetoka tofauti na msimu uliopita ambapo alikuwa anapata tabu kufanya 'sub' kwani waliokuwa ndani na walioko nje walikuwa na utofauti mkubwa kiuwezo.

"Nimeona nidhamu ya wachezaji wangu wapya na wa zamani mchezoni, kucheza pamoja, kufungua, kukimbia kwenye njia za mpira ni jambo muhimu na mimi nimelipenda, nafikiri nikiangalia sasa naona tunacheza kwa mfumo mmoja unaofanana, nimeona kipindi cha pili wakati tumebadilisha wachezaji, soka lilikuwa ni lile lile halikubadilika, hii inaonesha kabisa nina upana wa kikosi, kama nikifanya mabadiliko au kukiwa na majeruhi nina wachezaji ambao viwango vyao vinafanana, hii ni muhimu sana kwenye timu," alisema.

Akizungumzia mechi hiyo alisema muhimu kwake ilikuwa ni kuangalia wachezaji wake wa zamani na wapya jinsi gani wanacheza ili na yeye aongeze ufundi wake.

"Wachezaji wangu leo wameonesha soka safi, ufundi na staili ya kucheza, nafikiri kidogo kidogo, wiki kwa wiki tutakuwa kwenye kiwango cha juu kwa mashindano muhimu, leo (juzi), umeona tumecheza na wapinzani ambao tayari wao wamemaliza maandalizi yao ya msimu na wanarudi kwao kuanza ligi, kwa hiyo walikuwa vizuri sana kuliko sisi, Simba ndiyo imeanza muda si mrefu 'pre season,' ilikuwa mechi ya kirafiki na matokeo hayakuwa mabaya kwetu, kikubwa kwangu na benchi langu la ufundi ilikuwa ni kuangalia viwango vya wachezaji wetu wa zamani na wapya," alisema.

Bao la Simba liliwekwa wavuni na Kibu Denis, huku la Zira likifungwa na Rustam Ahmadzada.

Baadhi ya wachezaji wapya waliocheza mechi ya juzi ni Willy Onana, Febrice Ngoma, Aubin Kramo, na Che Fondon Malone.




Aliyekuwa kiungo mshambuliaji wa Simba, Msenegal Pape Sakho, wakati akitambulishwa mwishoni mwa wiki katika klabu yake mpya ya Quevilly Rouen Metropole (QRM) ya Ufaransa inayoshiriki Ligi 2 nchini humo. **PICHA: MTANDAO**

# Tanzania Wasichana U-18 waanza vema michuano Cecafa

Na Saada Akida

TIMU ya Taifa ya Tanzania ya Wasichana chini ya miaka 18 (U-18), imeanza vizuri katika mashindano ya kuwania ubingwa kwa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), baada ya jana kuibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Burundi.

Tanzania ni wenyeji wa mashindano hayo yaliyoanza rasmi jana katika Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam na kuibuka na ushindi huo kwenye mechi hiyo ya ufunguzi.

Timu zote zilifanya vizuri katika kipindi cha kwanza na kushindwa kupata matokeo, lakini dakika 45 za kipindi cha pili Tanzania iliongeza makali na kufanikiwa kuibuka na ushindi huo.

Kipindi cha pili Tanzania ilianza mpira wa kasi kwa kushambulia mara kwa mara katika lango la Burundi na dakika ya 64 ikajipatia bao la kwanza likifungwa na Winfrida Gerald kwa mkwaju wa penalti baada kipa wa Burundi kudaka miguu ya Zainabu Mohamed.

Dakika ya 71, Zainabu alikosa bao la wazi baada ya kushindwa kuweka mpira kambani akiwa anatazamana na nyavu.

Hata hivyo, Sarah Joel 'super sub' aliiandikia Tanzania bao la pili dakika ya 90 ya mchezo na kuifanya kuongoza kwa mabao 2-0.

Wakati watazamaji wakiamini mchezo huo umemalizika, dakika ya 92+, Aisha Juma aliweka kambani bao la tatu kwa mpira mrefu uliomshinda mlinda lango wa Burundi Amissa Inarukundo

Kikosi cha Tanzania katika mchezo huo kilikuwa ni Husna Zuber, Noel Patrick, Hasnath Linus, Joyce Fred, Winfrida Gerald, Ester Marwa, Aisha Juma, Zainabu Mohammed/Sara Joel, Dotto Evarist/ Diana William, Christer John na Vioeth Mwamakamba.

Kwa upande wa Burundi: Amissa Inarukundo, Chancelline Akimana, Emelyne Irankunda, Evelyne Akimana, Neema Nzohabonayo, Estella Gakima, Bora Inez, Rukiya Bizimana, Yasin Edgaridy, Adolphine Salum na Joella Akimana.

Tanzania itashuka tena dimbani kesho, Alhamisi dhidi ya Ethiopia mchezo huo ukipigwa tena katika Uwanja wa Azam Complex.

## Gamondi avimba droo michuano CAF

INATOKA UK. 24

shaji wa michuano yake ambapo kwa sasa hakutakuwa na faida ya timu inayotolewa raundi ya kwanza kwenye Ligi ya Mabingwa kuangukia mchezo wa mchujo wa mwisho wa Kombe la Shirikisho kuwania kutinga hatua ya makundi.

Utaratibu wa sasa timu itakayotolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika itakuwa imetoka jumla kwenye michuano ya msimu huu na itasubiri mpaka msimu ujao kama itafuzu.

Msimu uliopita Yanga ilitolewa kwenye raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Al Hilal ya Sudan kwa juma ya mabao 2-1, na kuangukia Kombe la Shirikisho ambako ilifanikiwa kutinga mpaka hatua ya fainali kabla ya kupoteza kwa idadi ya mabao 3-2 mbele ya USM Alger waliotwaa kombe hilo.

Katika droo ya jana, mabingwa hao watetezi wa Kombe la Shirikisho wanasubiri mshindi kati ya AS Loto ya Benin itakayocheza na Fath Union Sport (FUS) ya Morocco kuwania kutinga hatua ya makundi.

## Simba, Dynamos kusomana CAF mechi Simba Day

INATOKA UK. 24

katika Kilele cha Tamasha la Simba Day, ambalo mwaka huu, litafanyika Agosti 6, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Mabingwa hao wa Zambia watapamba siku hiyo maalum ya Simba kwa ajili ya kutambulisha wachezaji wao wa msimu mpya wa 2023/24, unaotarajiwa kuanza Agosti 15, ambabo mwaka huu kaulimbiu ya tamasha hilo litakalozinduliwa rasmi Buza Jumanne ijayo ni 'Unyama Mwingi'.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema kiingilio cha chini katika mchezo huo kitakuwa ni Sh. 5,000 mzunguko, Sh. 10,000 rangi ya machungwa VIP C Sh. 20,000, VIP B Sh. 30,000, VIP A Sh. 40,000 na Platinum Sh. 200,000.

Alisema katika jukwaa la platinum kutakuwa na viti 170 nusu ya fedha zitachukuliwa na kuongezewa katika ujenzi wa wodi za kinamama na watoto kwenye Hospitali ya Muhimbili na Mnazi Mmoja Zanzibar.

"Pamoja na lengo la kujenga wodi tutaanza na kuchangia damu kuanzia viongozi hadi matawi yote ya Simba sambamba na kufanya usafi katika jamii inayotuzunguka," alisema.

Ahmed alisema katika tamasha hilo wanatarajiwa kuwa na wasanii mbalimbali kutoka ndani na nje ya Tanzania kwa ajili ya kuwapa burudani Wanasimba kabla ya mechi.

"Baadhi ya wasanii wa ndani watakaokuwapo ni Tundaman, Meja Kunta, Whozu na wengine wataendelea kutambulishwa kadri siku zinavyoendelea," alisema Ahmed.

Aliongeza kuwa wameweka viingilio rafiki ili kila Mwanasimba kuweza kuvimudu kushuhudi wachezaji wapya ambao wamesajiliwa msimu huu.

"Tunahitaji kila Mwanasimba kufika uwanjani kuja kushuhudia timu yao na kuona wachezaji wetu tuliowasajili akiwamo Luis Miquissone, Willy Essomba Onana na wengine," alisema Ahmed.

Simba inafanya tamasha hilo kwa mara ya 15 msimu huu tangu lilipoanzishwa mwaka 2009.

Michezo
Jumatano Julai 26, 2023
Nipashe



## Mbappe aigomea PSG kutua Saudia
UKURASA 21



Gamondi
Robartinho

# GAMONDI AVIMBA DROO MICHUANO CAF

## Simba yawasubiri Wanamibia au Wazambia raundi ya kwanza kuwania hatua ya makundi...

**Na Faustine Feliciane**

LICHA ya Yanga kupangwa na 'kibonde' Asas FC ya Djibouti kwenye mchezo wa hatua ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika na ikivuka itakwenda kukutana na mshindi kati ya AS Otoho ya Congo dhidi ya Al-Merrikh ya Sudan, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema analijua soka la Afrika, hivyo aihofii timu yoyote.

Gamondi la Soka Afrika (CAF), jana lilifanya droo ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho, ambapo wawakilishi wengine wa Tanzania Bara, Simba wenyewe wataanzia raundi ya pili kwa kucheza ugenini na mshindi kati ya African Stars ya Namibia na Power Dynamos ya Zambia kuwania kutinga hatua ya makundi.

Wawakilishi wa wengine kutoka Zanzibar, KMKM yenyewe itacheza na St. George ya Ethiopia na mshindi wa mchezo huo atakutana na bingwa mtetezi, Al Ahly ya Misri kwenye hatua ya kwanza kuwania kufuzu hatua ya makundi.

Gamondi, aliliambia Nipashe jana kuwa hana hofu ya kukutana na timu yoyote na anaendelea kuiandaa timu yake ili kuweza kufanya vizuri kwenye michuano hiyo.

"Nafahamu kuhusu droo iliyochezeshwa, tumeona wapinzani wetu, lakini niseme tu tunajiandaa kukutana na timu yoyote na hakuna timu tunayoihofia, kikubwa ni kutumia muda wetu vizuri wa maandalizi," alisema Gamondi.

Endapo Yanga itafanikiwa kuwatupa nje Wadjibouti hao watasubiri kucheza na mshindi wa mchezo kati ya AS Otoho dhidi ya El Merreikh ya Sudan kuwania kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo mikubwa Afrika kwa ngazi ya klabu.

Kwa upande wa Kombe la Shirikisho Afrika, Singida Fountain Gate yenyewe itawakaribisha JKU ya Zanzibar katika mchezo wa hatua ya awali na mshindi wa mchezo huo atakutana na Future Club ya Misri kabla ya kutinga hatua ya makundi.

Azam FC wenyewe wameangukia kwa Bahir Dar Kenema ya Ethiopia katika mchezo wa awali na mshindi wa mchezo huo atakutana na Club Africain ya Tunisia, ambayo msimu ulioisha ilinyoshwa na Yanga katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kwenye michuano hiyo ya pili kwa utajiri barani Afrika.

Michezo ya mkondo wa kwanza kwa hatua ya awali itachezwa kati ya Agosti 18-20 na marudiano itachezwa kati ya Agosti 25-27, mwaka huu.

CAF imefanya marekebisho ya uwende-

UKURASA. 23

## Simba, Dynamos kusomana CAF mechi Simba Day

**Na Saada Akida**

WAKATI droo ya michuano ya Ligi ya Mabingwa iliyochezeshwa jana jijini Cairo, Misri na Shirikisho la Soka barani Afrika ikionesha mshindi kati African Stars ya Namibia na Power Dynamos ya Zambia atakutana na Simba kwenye raundi ya pili, Wekundu wa Msimbazi hao wamewaalika Wazambia hao kuvaana kwenye tamasha lao la Simba Day.

Mchezo huo utatoa nafasi nzuri kwa kila timu kuweza kusoma mbinu na uchezaji wa mwenzake kuelekea michuano ya Ligi ya Mabingwa ambayo raundi ya kwanza itaanza kutimua vumbi kati ya Agosti 18 -20, mwaka huu.

Simba inatarajia kuwakabili mabingwa wa Ligi Kuu ya Zambia,

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >